BREAKING NEWS
JACKPOT BABA LAO!
281,620,910/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Ajali** ilivyoua familia nzima papo hapo

UKURASA 2



**POGBA: NASUBIRI MATAJI NA JUVE**

UKURASA 22

Nipashe
Jumatano Julai 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581005 *
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Fundi umeme feki aua dada wa kazi

• **Mwili** auficha stoo, aiba fedha, adakwa baada ya kufanya ununuzi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**MWONGOZO UOMBAJI MIKOPO ELIMU YA JUU 2022/23 WAZINDULIWA**
SERIKALI imezindua mwongozo wa uombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2022/23 ambapo imetenga...

UKURASA WA 4
**TANROADS YATAJA SABABU MATUTA MENGI BARABARA YA KILWA**
WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umesema matuta yaliyowekwa katika Barabara ya Kilwa mkoani Dar es Salaam...

UKURASA WA 7
**MUHIMBILI YATANGAZA KIFO PACHA ALIYETENGANISHWA**
MMOJA wa pacha waliotenganishwa kwa operesheni maalum katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Neema, amefariki dunia...



Rais wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji Juxon Mlay (wa pili kulia), Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga (wa pili kushoto), Mjumbe wa Bodi ya MCT, Tido Mhando (kushoto) na Mkufunzi wa Vyombo vya Habari, Rose Mwalimu wakionyesha ripoti kuhusu mwongozo wa vyombo vya habari wa kuandika habari za watoto, wakati wa hafla ya uzinduzi wa machapisho manne ya baraza hilo, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

## Rais Samia: Ugonjwa wa ajabu waibuka Lindi

UKURASA 3





## Mzee wa miaka 89 abomoa nyumba zake watoto wasirithi

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC KUPAA MISRI KESHO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua ujenzi wa jengo la maktaba na ukumbi wa mihadhara wa Chuo cha Mwalimu Nyerere Kivukoni jijini Dar es Salaam jana, (wa pili kulia) ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, Makamu Mwenyekiti wa Chuo hicho, Mashavu Ahmada Fakh (kulia), Naibu Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi, Steven Wasira na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Fransic Maiko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Fundi umeme feki aua dada wa kazi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia mkazi wa Kimara Temboni, Mtaa wa Amani, Selemani Haruna, maarufu Kwata (24), kwa tuhuma za kumuua msichana wa kazi za ndani, Editha Charles (22) na kuuficha mwili katika stoo ya vifaa vya ujenzi katika nyumba ya Agatha Stanslaus.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini hapa jana, alisema uchunguzi wa awali umeonyesha Julai 6 mwaka huu, majira ya asubuhi, mtuhumiwa alifika kwenye nyumba aliyokuwa anaishi binti huyo wa kazi, akijifanya fundi wa umeme na alitakiwa kuweka balbu.

"Alipoingia ndani, alimshambulia kwa kitu chenye ncha kali binti huyo na kumuua halafu akavunja chumba cha mwenye nyumba na kuiba Sh. milioni 1.8 na kutoweka.

"Polisi kwa kutumia wataalamu wake wa uchunguzi wa kisayansi na vyanzo vingine vya kiuchunguzi, walibaini mtuhumiwa huyo kuwa aliingia kwenye nyumba hiyo na kukaa kwa saa kadhaa na kutoka.

"Baada ya kumkamata na kumhoji kwa kina, alikiri kumuua binti huyo, kuvunja mlango wa chumba na kuiba fedha hizo na mwili wa marehemu aliuficha kwenye stoo ya nyumba hiyo huku akiwa ameufunika na vifaa mbalimbali vya ujenzi ili usionekane," alisema.

Kamanda Muliro alisema mtuhumiwa huyo ameonyesha kiasi cha fedha alizoziiba eneo hilo na zingine alidai mara baada ya tukio, siku iliyofuata alinunua vitu mbalimbali zikiwamo simu mpya aina ya Infinix, viatu vya mpira jozi mbili na begi la mgongoni lenye nguo mbalimbali mpya ambavyo navyo vimepatikana. Kamanda Muliro alisema kitendo alichofanya mtuhumiwa ni cha kikatili na uchunguzi wa shauri hilo unakamilishwa ili afikishwe mahakamani.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linamshikilia Jonas Ziganyige (71) ambaye ni mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na mkazi wa Mbezi Juu kwa tuhuma za kumpiga risasi na kumuua Patient Romwadi (48), mfanyabiashara na mkazi wa Wazo Mivumoni, Kinondoni.

"Taarifa za awali zinaonyesha kuwa Julai 9 mwaka huu, majira ya saa nne asubuhi, Recy Renso (52), mkazi wa Posta alifika eneo hilo na mtu huyo ambaye ni marehemu kwa sasa kwa lengo la kuangalia mipaka ya kiwanja chake. "Mtuhumiwa alitoka ndani huku akionyesha kukasirishwa na hatua ya watu hao, akachukua bunduki na kumpiga risasi Patient Romward ambaye baadaye alifariki dunia.

"Baada ya tukio hilo, mtuhumiwa alikimbia lakini upelelezi ulifanywa haraka na Julai 10 mwaka huu alikamatwa eneo la Kibaha Maili Moja akiwa amejificha," alisema.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limeipata silaha aliyotumia mtuhumiwa ambayo ni aina ya Mark IV ikiwa na risasi nne.

"Mtuhumiwa atafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo kujibu mashtaka yanayomkabili. Jeshi la Polisi linaendelea pia na jitihada za kuzuia vitendo vya kihalifu kwa kufanya operesheni kali inayoongozwa na taarifa fiche dhidi ya uhalifu na wahalifu katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

"Watuhumiwa wanane sugu wa uvunjaji nyumba na kuiba vifaa vya magari akiwamo Jumanne Omary (28), mkazi wa Mikwambe na wenzake saba, wamekamatwa wakiwa na Tv flat screen nne za aina ya mbalimbali, kompyuta mpakato mbili, sabufa moja, simu aina mbalimbali tano pamoja na vifaa vya kutendea uhalifu vikiwamo mikasi miwili mikubwa ya kuvunjia, panga moja, kisu kimoja, prize na bisibisi, tochi na nyaraka mbalimbali.

Pia alisema wamekamata gari lenye namba za usajili T 787 DGW aina ya Toyota Gaia, likihusishwa na kutumiwa kwenye vitendo vya kihalifu.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuacha kujihusisha na vitendo vya kihalifu kwani kwa kufanya vitendo hivyo watakamatwa na watajikuta wakiwa katika msuguano mkali wa kisheria na vyombo vya dola," alisema.

# Ajali ilivyoua familia nzima papo hapo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WATU wanane wamefariki dunia katika ajali iliyohusisha magari mawili katika eneo la Busiri, barabara kuu ya Lusahunga kuelekea Kata ya Nyakahura wilayani Biharamulo mkoani Kagera.

Magari yaliyohusishwa kwenye ajali hiyo ni lori lenye namba za usajili RAF 129W ambalo liligongana na gari dogo aina ya Mercedes Benz lenye usajili namba T.626DRX lililokuwa limebeba familia ya watu watano.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo ambayo ilitokea juzi majira ya saa moja usiku katika eneo la Busiri barabara kuu kutoka Lusahunga kuelekea Kata ya Nyakahura wilayani Biharamulo mkoani humo.

Mwampaghale alisema lori hilo lilikuwa likiendeshwa na Vicent Ogakuba (52) raia wa Rwanda, likitokea nchini humo kwenda mkoani Dar es Salaam.

Alisema gari dogo lilikuwa likiendeshwa na Nyawenda Bihela (35), mkazi wa Kijiji cha Kikoma katika Kata ya Lusahunga, wilayani Biharamulo ambaye alikuwa akielekea Kijiji cha Nyamalagala, wilayani Ngara.

"Huyu dereva wa gari dogo alikuwa amekodiwa usiku na mama mwenye watoto wanne ndipo akatafuta watu wawili wa kumsindikiza kwani ilikuwa majira ya usiku na alifanya hivyo kwa kuhofia usalama wake," alisema Kamanda.

Kadhalika, alisema katika ajali hiyo watoto wanne wa familia moja na mama yao walipoteza maisha akiwamo dereva wa gari dogo na watu wengine wawili waliokuwa wakimsindikiza katika safari hiyo.

Alitaja majina ya marehemu hao kuwa ni Nyawenda Bihela (35), dereva ambaye pia alikuwa mmiliki wa gari dogo, Michael Charles (28) na Majaliwa Kanundo (32).

Alitaja marehemu wengine kuwa ni pamoja na watoto wa familia moja ambao waliokuwa wakisafiri na mama yao kwenda wilayani Ngara kuwa ni Magreth Sekanabo (14), Adidas Sekanabo (12), Zabron Sekanabo (6), Vestina Sekanabo (4) na mama yao Jesca Leonard (45).

Kamanda alisema, chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa gari kubwa lililokuwa likitokea nchini Rwanda baada ya kuhama upande wa kushoto wa barabara kuamua kupita kulia.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa chumba cha kuhifadhia maiti kwenye kituo cha afya Nyakanazi na dereva wa gari kubwa amekamatwa na atafikishwa mahakamani.

# Mzee wa miaka 89 avunja nyumba zake za mil. 200/-

**Na Thobias Mwanakatwe**

MZEE mwenye umri wa miaka 89, Iddy Maganga, ameamua kuvunja nyumba zake mbili zenye thamani ya Sh. milioni 200, eneo la Ngarenaro NHC jijini Arusha kwa madai baadhi ya watoto wake wanataka kumdhulumu ili wazimiliki.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe, Mzee Maganga alisema katika kutekeleza kile alichokiita mpango wa kutaka kumuua, mmoja wa watoto wake alimfungia ndani kwenye chumba chenye giza nene kwa muda wa wiki moja, bila kumpa chakula wala mahitaji muhimu na kulazimika kula kinyesi chake. Maganga alisema nyumba zake alizijenga na mke wake ambaye alishafariki dunia.

"Niliamua kuzivunja nyumba hizo kwa kukodi watu ambao niliwalipa baada ya kubaini kwamba baadhi ya watoto wangu wakiongozwa na Abdalah Maganga wanania ovu juu ya mali zangu," alisema.

Aliongeza kuwa alichukua uamuzi huo akiwa na akili timamu na amefanya hivyo ili kuwakomesha watoto wasiotaka kufanya kazi, wakisubiri mali za urithi kutoka kwa wazazi wao.

"Hii nyumba ni mali yangu, nilijenga na mke wangu ambaye kwa sasa ni marehemu, huyu mtoto Abdalah alinifungia ndani wiki moja nikiwa nakula kinyesi changu sijitambui na nilikuja kuokolewa na mtoto wangu wa kike aitwaye Jasimin na mume wake baada ya kuvunja kitasa na kunitoa na kunipeleka hospitali," alisema.

Akisimulia zaidi, alisema jirani yake aliyemtaja kwa jina la mama Masawe ambaye alikuwa akienda kuchukua chakula kwake, alimpigia simu mtoto wake Jasimin na kumwambia kuwa mzee Abdalah haonekani siku ya nne.

Baada ya taarifa hizo, binti yake na mume wake walikwenda nyumbani na kumkuta akiwa amefungiwa ndani hajitambui kutokana na njaa.

Mzee Maganga mwenye watoto sita, kwa sasa anaishi kwa mtoto wake eneo la Kwa Mrombo, akidai kuwa Abdalah alikuwa na nia mbaya juu yake, kutaka afariki dunia ili ajimilikishe nyumba hiyo kinyume cha sheria.

Alisema, licha ya kuwa hiyo nyumba ni mali yake, lakini mtoto wake alikuwa hamruhusu baba yake kuingia ndani ya nyumba hiyo na anapokuwa akitaka msaada kwa kijana huyo, alikuwa akifunga milango na geti.

Mzee Maganga aliwataka Abdalah na Mwenzake Ridhiki Maganga kukaa mbali na mali zake wakatafute mali zao na kwamba baada ya kubomoa nyumba hiyo ana mpango wa kuliuza eneo hilo.

"Baada ya kupata fahamu nilianza taratibu za kuuza nyumba yangu, lakini kila nikifika na mteja nafungiwa nje na mwanangu Abdalah, hataki niingie ndani hata kujisaidia," alilalamika.

Jasimin, akizungumzia tukio hilo la baba yake, alisema alimwokoa akiwa kwenye hali mbaya baada ya kumkuta hajitambui na amefungiwa kwenye chumba kidogo kwa wiki moja bila kupatiwa chakula wala maji.

"Nilimkuta baba yangu akiwa kwenye hali mbaya sana alikuwa haongei, chumba kilikuwa na giza kimefungwa na kinanuka kinyesi na alikuwa akila kinyesi chake, nilimpeleka hospitali na baada ya kupatiwa matibabu alipata nafuu na kurejea katika hali ya kawaida na sasa naishi naye," alisema.

Mtoto anayetuhumiwa kufanya tukio hilo, Abdalah Maganga, alikanusha taarifa za kumfungia baba yake kwenye chumba kwa wiki nzima bila chakula, akidai kuwa taarifa hizo hazina ukweli.

Abdalah alikiri kuwa nyumba hiyo ni mali ya baba yake na marehemu mama yake na yeye alikuwa akiishi hapo kama mwangalizi.

Alisema ameshtushwa kuona kundi la watu zaidi ya 50 kuvamia nyumba hiyo siku ya Jumamosi wiki iliyopita na kufanya uharibifu.

Alisema baada ya kundi hilo kuvamia alijitahidi kutafuta msaada polisi, lakini hakupata kwa wakati na walipofika kuchelewa walikuta nyumba zote zimevunja na vitu kutolewa nje.

"Mimi sina ugomvi na baba yangu ila sina mawasiliano naye kwa muda baada ya kuchukuliwa na kuishi na mdogo wangu Jasimin, nitakachofanya kwa sasa ni kumwachia Mungu tu," alisema Abdalah.

Hata hivyo, mdogo wake Mzee Maganga, Hasan Abdalah, alisema hana mawasiliano na kaka yake na kushauri kuwa kitendo kilichotokea kinapaswa kumalizika kisheria mahakamani.

## Mwongozo uombaji mikopo elimu ya juu 2022/23 wazinduliwa

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imezindua mwongozo wa uombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2022/23 ambapo imetenga Sh. bilioni 573 kwa ajili ya mikopo hiyo.

Mbali na makundi mengine, mikopo hiyo itatolewa kama ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Katika hafla ya uzinduzi wa mwongozo huo mkoani Dar es Salaam jana, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliwaambia waandishi wa habari kuwa serikali imeongeza kiwango cha fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili wote wenye uhitaji wa kupata mikopo, waipate na kutimiza malengo yao ya kujiendeleza kielimu.

"Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. bilioni 573. Kati yake, Sh. bilioni 570 zitatolewa kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na Sh. bilioni tatu zitatumika kuwafadhili wanafunzi waliofaulu vizuri masomo yao ya sayansi kidato cha sita ambao watadahiliwa kusomea masomo ya sayansi, uhandisi na elimu tiba katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali.

"Mwongozo wa uombaji mikopo hiyo utapatikana kuanzia Julai 13 (leo) katika tovuti ya bodi ya mikopo na kuanzia Julai 19 hadi Septemba 30, dirisha la kuomba mkopo litakuwa wazi kupokea maombi ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu," alifafanua.

Vilevile, aliwataka wanafunzi wenye uhitaji, kupunguza makosa katika uombaji wa mikopo ili kuepuka kujiweka katika hatari ya kukosa mkopo ilhali wanazo sifa.

"Kwa hiyo, tutaendelea kutoa mafunzo juu ya uombaji wa mikopo. Awamu hii hatutaki kuona makosa yanajirudia katika uombaji wa mikopo.

"Mafunzo yetu tutayafanya kupitia vyombo vya habari, mikutano mbalimbali na kupitia katika vyuo mbalimbali kutoa elimu ili wanafunzi wasifanye makosa ambayo yatasababisha kukosa mkopo," alisema Prof. Mkenda aliipongeza NMB kwa kutenga Sh. bilioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba ndogo ya asilimia 10 kwa watumishi walioko serikalini lakini wanajiendeleza kielimu na kutoa wito kwa benki zingine kuiga mfano huo.

"Ninaipongeza Benki ya NMB kwa hatua hiyo nzuri. Ninaamini itasaidia watumishi na wanafunzi wengi kujiendeleza kielimu.

"Katika kuunga mkono jitihada za serikali katika sekta ya elimu, NMB pia imetenga fedha na kompyuta kwa ajili ya kuwafadhili wanafunzi 100 wa elimu ya juu," alipongeza.

Waziri huyo pia alimpongeza Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, kwa kutenga nafasi 50 za kuwafadhili wanafunzi 50 waliofaulu vizuri masomo ya sayansi, akiwasomesha kwa fedha zake mwenyewe.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Prof. Hamisi Dihenga, alimwahidi Waziri Mkenda kuwa watafanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kila aliyeomba mkopo anatimiza vigezo na kupata mkopo kwa wakati.




Balozi wa Uturuki nchini Tamzania, Mehment Gulluoglu (wa pili kushoto), akimshika mtoto mwenye ualbino wakati wa ugawaji wa nyama katika shughuli iliyoratibiwa na Taasisi ya Rehema kwa ushirikiano na Taasisi za Kituruki ili kusherehekea sikukuu ya Eid el Adha na makundi mbalimbali ya watu wenye mahitaji maalumu. Kushoto ni Kiongozi wa Kizlay, Yusuf Ramazan, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia: Kuna ugonjwa wa ajabu umeibuka Lindi

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amemtaarifu kuwa mkoani Lindi kuna ugonjwa wa ajabu umewakumba wananchi wake ambao wanatokwa damu puani na hata kudondoka.

Amesema tayari timu ya wataalamu wa afya na wa sayansi wameshakwenda huko kwa ajili ya kuchunguza ugonjwa huo.

Rais Samia alibainisha hayo jana katika mkutano wa 20 wa Shirikisho la Baraza la Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati (AMECEA) ambao unafanyika nchini kuanzia Julai 8-18 mwaka huu.

Mkutano huo wenye kaulimbiu 'Athari za mazingira katika maendeleo ya binadamu', unashirikisha viongozi hao wa kiroho kutoka nchi za Eritrea, Ethiopia, Sudan Kusini, Kenya, Somalia, Djibouti, Uganda, Tanzania, Zambia na Malawi.

Katika mkutano huo jana, Rais Samia alisema kuna maradhi ambayo huko nyuma walikuwa hawayajui kwa sababu hayakuwapo, lakini kutokana na uharibifu wa misitu, viumbe vilivyopo huko vinasambaa.

"Kuna kila aina ya maradhi mapya yanazuka ambayo hatujayajui. Nilikuwa ninazungumza na Waziri Mkuu, juzi alitoka ziara kusini, Lindi, ananiambia ameona kuna maradhi yameingia wanadamu wanatokwa tu damu za pua na wanadondoka.

"Hatujui ni kitu gani, wanayasansi, wataalamu wa afya wote wamehamia huko wanaangalia ni kitu gani. Kwanini mwanadamu atokwe tu na damu kwenye pua, adondoke? Angekuwa mmoja, wawili tungesema presha imepanda lakini ni wengi kwa mfululizo," alibainisha.

Rais Samia alisema ni maradhi ambayo hawajawahi kuyaona na yote ni kwa sababu wanaharibu makazi ya viumbe kule walikoumbwa na Mungu misituni.

Alisema wanawasogeza viumbe hao kwao na kusababisha aina tofauti za maradhi.

Mkuu wa Nchi pia alisema vita na migogoro ni sehemu ya uharibifu wa mazingira, akisisitiza kuwa kuwa wanapaswa kuhakikisha wakati wote kunakuwa na amani.

Aliwapongeza viongozi hao wa kiroho kwa kuchagua mada hiyo muhimu ya mazingira kwa mataifa yao na utayari wa kushirikiana na serikali katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira kwa sababu vita hiyo siyo ya mtu mmoja.

Pia alisema wameamua kutekeleza kwa vitendo mambo ambayo wameamrishwa na ulimwengu kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

"Lengo la 17 ambalo ndilo ninawapongeza linasema tufanye umoja katika kutekeleza haya malengo ambayo tunayatekeleza, ninawashukuru sana, mmefikiria na mkitoka hapa mnakwenda kutekeleza kwa vitendo malengo ya dunia na ya Afrika ambayo tumeelekezwa kufanya, hongereni sana makadinari na viongozi wote wa dini," alisifu.

Rais Samia alisema inatia moyo kuona Baba Mtakatifu Francis ambaye ameona inafaa suala la utunzaji wa mazingira kuwa sehemu ya ujumbe na mpango mkakati ili lipate msukumo zaidi.

"Kama alivyoeleza Baba Mtakatifu dunia ni yetu sote, hakika sisi Tanzania tunathamini maisha ya kijamii, yanayoendana mantiki ya mkakati huo wa Kanisa Katolini kwamba sasa, tujenge nyumba yetu sote, tuitunze nyumba yetu sote, tulinde mazingira na tuyatunze ili dunia iwe njema kwa maisha ya leo na ya kesho ya vizazi vijavyo," alihimiza.

Pia alipongeza namna wanavyoshiriki kutunza mazingira katika maeneo yao na kuwaomba wawaelimishe waumini ili nao wafanye hivyo.

Rais Samia aliwaeleza kuwa wanapenda kupata maazimio yao watakayofikia ili kuona namna gani watayaweka kwenye sera ili wote watekeleze na kuliinda dunia.

Rais wa AMECEA, Askofu Charles Kasonde, alisema ipo haja kunusuru uharibifu wa mazingira unaoendelea ili kuifanya dunia kuwa sehemu salama.

Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga wa Jimbo Kuu la Mbeya, alimshukuru Rais kwa kuwezesha kufanyika kwa mkutano huo kwa amani na wageni wote wamefurahia kuwapo Tanzania.

Alisema ajenda ya mkutano huo inarejea kauli ya Papa Francis aliyoitoa mwaka 2015 kwamba wana wajibu wa kulinda mazingira waliyonayo kama nguzo ya uhai wa binadamu na wao kama maaskofu wanaahidi kuunga juhudi za kimataifa za kulinda mazingira.

# Wapinga serikali kuunda Bodi ya Ithibati ya Habari

**Na Mary Geofrey**

WADAU wa habari nchini wametaka uundwaji wa Bodi ya Ithibati ya Habari huru, ili kuweka mazingira ya usawa kati ya serikali na vyombo vya habari nchini.

Mjumbe wa Kamati Tendaji wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Nevile Meena, ni mmoja wa wahariri waliowasilisha maoni hayo kuhusu kuundwa kwa bodi hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam.

Meena alisema iwapo serikali itaamua kuunda Bodi ya Ithibati ya Habari, bodi hiyo itakosa uhuru wa kufanyia uamuzi malalamiko yatakapoihusu serikali.

"Bodi ya Ithibati ya Habari ikisimamiwa na serikali, itakosa uhuru wa kuamua. Hiyo, bodi inapaswa kuundwa na wanataaluma na kazi yake ni ya kitaaluma. Serikali ikiwa na malalamiko nayo inakwenda kulalamika kwenye bodi na wala haipaswi kutoa maelekezo," alisema Meena.

Mhariri wa Gazeti la Raia Mwema, Joseph Kulangwa, alisema ana wasiwasi iwapo serikali itasimamia uundwaji wa bodi hiyo.

"Serikali itataka iandikwe vizuri tu, ndiyo wahalalishwe kufanya kazi hiyo," alisema Kulangwa.

Alisema, tasnia mbalimbali nchini zimeunda na kusimamia bodi zao wenyewe bila maelekezo au kuingiliwa na serikali na kuhoji sababu za serikali kupendekeza kuunda bodi hiyo badala ya kuwaacha wanataaluma wa habari kuunda na kuisimamia.

Mhariri wa Jarida la Tz & Beyond na PANAROMA, Jimmy Charles, alisema, iwapo serikali itaunda bodi hiyo, itajihakikishia uhuru wa habari kuwa mikononi mwake.

"Ikumbukwe kuwa, kwa sasa serikali ndiyo mwamuzi wa mwisho kwa maana ya kuwa ndiyo mlalamikaji, msikilizaji na hakimu kwa wakati mmoja. Na ukitaka kujua hilo, utaona pale tu utakapogusa kile isichopendezwa nacho (serikali). Tasnia ya Habari inahitaji bodi huru isiyosimamiwa na serikali," alisisitiza.

Mei 31, mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema, serikali inaendelea na taratibu za kuanzisha Bodi ya Ithibati itayokuwa na jukumu la kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari wenye sifa.

Alisema, Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, inaelekeza kuanzishwa kwa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari pamoja na mfuko wa mafunzo kwa wanahabari.

Kwa upande wa Jaji Eliezer Feleshi, ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), alisema ni vizuri kwa Bodi ya Ithibati ya Habari ikaundwa na kusimamiwa na wanahabari wenyewe.

Alitoa maoni hayo Mei 13, mwaka huu, wakati alipokutana na wadau wa habari ofisini kwake bungeni, jijini Dodoma.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel (kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila (kushoto), Mwenge huo ulipokelewa jana mkoani Mwanza na utakimbizwa mkoani humo mpaka Julai 19, utakapokabidhiwa mkoani Geita. **PICHA: RICHARD MAKORE**

## Mkemia atoa elimu udhibiti uagizaji wa kemikali nchini

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amesema wanaendelea kutoa elimu kuhusu udhibiti uagizaji na uingizaji wa kemikali ambazo ni malighafi za viwanda ili kuepuka madhara yanayosababishwa na matumizi holela.

Dk. Mafumiko alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika Viwanja vya Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara, alipozungumza na wananchi waliotembelea banda la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kujifunza shughuli wanazofanya.

Alisema jukumu lao ni kuelimisha jamii, hasa wawekezaji wa sekta ya viwanda na biashara ambao wanaagiza kemikali kutoka nje ya nchi, kufahamu aina ya kemikali zinazoagizwa, namna ya kuhifadhi na matumizi sahihi.

"Tunafanya kila linalowezekana kwa njia ya mtandao lakini ana kwa ana, kuzungumza na wateja ili kuwaeleza mahitaji gani yanayohitajika kuwekeza katika kemikali. Na tunatambua kwamba ukiwekeza kemikali, ina faida sana katika viwanda nchini, hivyo sisi tunadhibiti matumizi holela,"alisema.

Dk. Mafumiko alisema wanatoa elimu kwa wananchi wanaotaka kuwekeza katika sekta hiyo ili kufahamu aina ya kemikali zinazohitajika nchini kabla ya kuagiza mzigo na hata baada ya kuwasili, hukagua.

Alisema pia wanafanya uchunguzi wa kimaabara kuhakikisha ubora wa bidhaa zinazokwenda kushughulika na kemikali.

"Ujumbe wangu muhimu ni kwamba wadau wote wanaopita kwenye banda letu, wapate elimu sahihi kuhusu utumiaji wa kemikali kama malighafi na hasa inayoenda kutumika katika uzalishaji wa viwanda," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema huduma zingine wanazotoa ni za uchunguzi wa vinasaba vya binadamu (DNA) kwa gharama ya Sh. 100,000.

"Mara nyingi nimekuwa nikisikia gharama za Mkemia Mkuu wa Serikali za kuchukua hivi vipimo ni Sh. millioni mbili, Sh. 500,000, Sh. 700,000, hiyo ni taarifa ambayo siyo sahihi," alisema.

# TANROADS yataja sababu matuta mengi 'Kilwa Road'

**Na Martha Magawa**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umesema matuta yaliyowekwa katika Barabara ya Kilwa mkoani Dar es Salaam siyo ya kudumu, bali yanalenga kupunguza vifo vya wanafunzi na ulemavu uliokuwa ukisababishwa na madereva wasio waadilifu.

Umesema madereva hao wamekuwa wakisababisha vifo na ulemavu kwa wanafunzi wanaovuka barabara hiyo kwenda shuleni na wanaporejea majumbani.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senkuku, katika mazungumzo mahususi na Nipashe ofisini kwake jana kuhusu suala hilo, alisema matuta hayo hayatatumika kwa muda mrefu, hivyo akawataka watumiaji wa barabara waendelee kuvumilia mpaka mkandarasi atakapokamilisha ujenzi.

Alisema watoto ndiyo walikuwa waathirika wakubwa wa ajali za barabara hiyo, jambo lililoisukuma TANROADS kutafuta dawa ya kumaliza tatizo hilo.

"Kesi za watoto wa shule (wanafunzi) kugongwa zilikuwa nyingi katika eneo lile, hivyo ikatulazimu kuja na mbinu mbadala ya kuokoa maisha ya watoto wale.

"Ni kweli kuna foleni lakini wavumilie mkandarasi amalize kazi, tuhamie hatua nyingine," Meneja huyo alifafanua.

Senkuku aliongeza kuwa TANROADS inatambua matuta yameongeza foleni kwa kupunguza kasi ya magari, hivyo akaahidi kuwa ujenzi ukikamilika, yataondolewa na kuwekwa taa za barabarani ambazo zitasaidia kupunguza ajali.

Akifafanua zaidi kuhusu suala hilo, meneja huyo alinyoshea kidole tatizo lililopo katika barabara za Tanzania kwamba zinatumika kwa matumizi yote ambayo ni ya vyombo vya moto na binadamu.

Alisema hicho ndicho kimeisukuma serikali kuongeza madaraja ya juu ili kupunguza vifo vya watembea kwa miguu.

"Watembea kwa miguu pamoja na machinga pembezoni kwa hifadhi za barabara jijini kwetu ilikuwa tatizo pia, lakini tunashukuru zoezi la kuwaondoa machinga limefanikiwa kwa kiwango kikubwa," alipongeza.

Akizungumzia nidhamu ya watumiaji wa barabara hasa katika vivuko, meneja huyo alisema kuwa bado wananchi hawatumii madaraja ya juu kutokana na kutotii sheria, hivyo wengine husababisha ajali na madhara mengine kwao wenyewe.

"Madaraja ya juu wananchi wamekuwa wavivu kuyatumia na kulazimisha kuvuka chini. Ili kukomesha tabia hizo, tumezungushia nyavu maeneo yote yenye madaraja na muda siyo mrefu utaanza ujenzi wa barabara za juu katika maeneo mengi ikiwamo Mwenge," alidokeza.

Kwa mujibu wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, mwaka huu serikali inatarajia kuendelea na ujenzi wa barabara za juu mkoani Dar es Salaam kwenye maeneo ya Fire, Magomeni, Tabata na Mwenge.

## Burundi yavutiwa na masoko ya machinga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU wa Chama Tawala Burundi (CNDD-FDD), Reverien Ndikuriyo, amepongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuweka miundombinu mizuri kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga.

Ndikuriyo alitoa pongezi hizo jana alipotembelea na kuangalia Soko la Machinga linalojengwa katika Jiji la Dodoma.

"Nilipofika hapa nilikuwa ninahoji mamantilie wamewekwa wapi? Hakika mmewajali wafanyabiashara wadogo. Tulikuwa tunasikia machinga wanapewa vitambulisho kwa Sh. 20,000 na sasa mnawawekea miundombinu hii, mmefanya jambo jema, nasi tutajifunza kupitia ubunifu huu," alipongeza. Akiwa katika kiwanda cha mbolea cha Intracom kinachojengwa na mwekezaji kutoka Burundi kwa gharama ya dola za Marekani milioni 180 ambacho kitakuwa na uwezo wa kutoa ajira 3,000, kiongozi huyo aliwapongeza marais wa Tanzania na Burundi kwa kudumisha demokrasia ya uchumi.

"Hatua hii imefanya kujengwa kiwanda cha mbolea ambacho ni kikubwa zaidi ya kilichoko Burundi ambacho kwa sasa kuna mpango wa kukipanua zaidi.

"Kiwanda hiki ni fursa nzuri ya kutoa ajira kwa ndugu zetu vijana wa Kitanzania, na tumeona jinsi vijana wasomi wetu kutoka kwenye vyuo vyetu kama UDOM wanaoongeza utaalamu wa kuweka viwango sawa katika kuzalisha mbolea, hii ni hatua kubwa sana kwa nchi zetu," alisema.

Ndikuriyo pia alitembelea Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Stendi ya Kisasa ya Mabasi na kiwanda cha mvinyo, akisema katika miaka 60 ya uhuru, Tanzania imezidi kupiga hatua na imepiga hatua ya maendeleo kutokana na usalama uliopo.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Christina Mndeme, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisimamia demokrasia ya uchumi na serikali chini ya CCM imeendelea kuhakikisha kuna mazingira mazuri ya uwekezaji.

Alisema kiwanda hicho kinakwenda kuongeza mapato kupitia mnyororo mzima wa uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea hiyo.

"Wito wangu kwa wafugaji kwa uwekezaji huu, kinyesi cha mifugo ni mali, hivyo ni vyema kuanza kujipanga kufuga zaidi ili kuzalisha bidhaa hizo kwa wingi na ambazo zitakuwa kwa asilimia kubwa malighafi kwa kiwanda hicho," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema uongozi wa mkoa utahakikisha huduma muhimu zinazotakiwa zinapatikana pindi uzalishaji utakapoanza.

Awali, Mhandisi wa Intracom, Emmanuel Ngowi, alisema ujenzi wa kiwanda hicho unaendelea vizuri na kuwa awamu ya kwanza ya uzalishaji inaanza muda wowote ndani ya mwezi huo, huku Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa Intracom, Ntukamazina Nepomuscene, akisema mbolea hiyo imefanyiwa majaribio na kuonyesha matokeo mazuri kwenye mazao ya mahindi, alizeti, maharage, mpunga na mtama.

# Wizara yasisitiza umakini mitaala, sera mpya elimu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara hiyo haihitaji kukurupuka bali kuwa na utulivu katika kuandaa mitaala na sera mpya ya elimu.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akiweka jiwe la msingi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Kigamboni inayojenga jengo la ghorofa tatu ambalo ndani yake, kutakuwa na maktaba yenye uwezo wa kuchukua watu 2,500.

Jengo hilo ambalo linajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 14.9, pia litakuwa na ukumbi wa mihadhara utakaochukua watu 1,000, ofisi za wafanyakazi na kumbi ndogo za mikutano za watu 200 hadi 250.

"Hatutaki kukurupuka, tumekubaliana hatuingii Wizara ya Elimu kukurupuka, haiwezi ikawa Wizara ya Elimu akija (Dk. Shukuru) Kawambwa kulia geuka, akija (Prof. Joyce) Ndalichako kushoto geuka, akija (Prof. Adolf) Mkenda nyuma geuka, akija mwingine mbele tembea, hatutafika.

"Tumekubaliana Wizara ya Elimu ni wizara inayohitaji utulivu, umakini. Kuna watu wakiona hawajui, ukiona kobe kanyamaza, anatunga sheria, kazi inayofanyika," alisisitiza.

Prof. Mkenda alikumbusha kuwa ubora wa elimu ni ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameshaweka bayana kwamba anahitaji mageuzi katika sekta hiyo ili elimu iongeze ubora na iakisi mahitaji ya nchi.

Kuhusu ujenzi huo, Prof. Mkenda alikipongeza chuo hicho kwa hatua hiyo inayofanya na kumpa nafasi yeye kuweka jiwe la msingi chuoni huko.

"Kama alivyosema mkuu wa chuo, fedha za bajeti zimekuwa zikitengwa mwaka nenda mwaka rudi lakini kuwapo kwenye bajeti ni jambo moja na kutoka ni jambo lingine," alisema.

Waziri huyo alisema chini ya uongozi wa bodi ya chuo hicho ambayo Mwenyekiti wake ni Stephen Wassira na Mkuu wa Chuo, Prof. Shadrack Mwakalila, wamehakikisha wanatumia fedha za ndani kuanza ujenzi bila kusubiri.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Mwakalila, alisema hivi karibuni wanatarajia kutoa Shahada ya Uzamivu (PhD) na kwamba wameshaweka mkakati wa kuboresha miundombinu ya chuo.

"Wanafunzi lazima wasome katika mazingira mazuri. Tuna asilimia 40 ya bajeti ya mapato ya ndani ambayo tumetenga ili kufanikisha uboreshaji wa miundombinu. Fedha hizi zinatokana na ada za wanafunzi wanazolipa.

"Kwa kutenga asilimia 40 tumekwamua ujenzi uliokwama wa hosteli kule Zanzibar ambazo mwaka jana Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alizindua ujenzi wake ambao kwa sasa umefikia asilimia 40 na ujenzi wake unagharimu Sh. bilioni 15.2. Kule tunajenga pia nyumba za wafanyakazi ambazo ni shida," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi wa Chuo hicho, Wassira, alisema wamefundisha vijana wengi vyuoni lakini wakitoka hawajui cha kufanya.

Alisema ni lazima mfumo wa elimu uhakikishe unawapa wanafunzi ujuzi wa kujitegemea ambao utawaelekeza wapi pa kwenda katika mazingira haya mapya.

Wassira alisema ili kujenga nchi na watu wake, mapinduzi katika elimu ni jambo la msingi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kushoto), akipatiwa maelezo kuhusu kifaa kinachoonyesha ukuaji wa kifaranga ndani ya yai mpaka siku kitakapototolewa alipotembelea shamba la Ogania wilayani Kibaha, mkoani Pwani. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Wanaoharibu misitu kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi

**Na Beatrice Shayo**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, amewataka wanaokata miti kiholela na kuharibu mazingira kuacha mara moja au watakabiliwa na kesi za uhujumu uchumi.

Silayo aliyasema hayo jana wakati akihojiwa na Nipashe kuhusu ukataji wa miti kiholea unaoendelea katika baadhi ya maeneo.

Alisema sheria zipo wazi unapokata miti kiholela bila utaratibu ni kosa la jinai unapaswa kukamatwa na kufikishwa kwenye ngazi za mahakama.

Anayepatikana na hatia anaweza kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili au kulipa faini kutokana na mahakama itakavyoona uharibifu uliofanywa na mtuhumiwa.

"Kwa uharibifu aliofanya anaweza pia kushtakiwa kwa kesi ya uhujumi uchumi kulingana na kiwango cha uharibifu alichokifanya na anaweza kulipa gharama za kiwango cha uharibifu na kuhukumiwa kifungo," alisema Silayo. Alisema jambo hilo limefanyika na wapo wengi walioshtakiwa kwa kosa la uhujumu uchumi kutokana na ukataji wa miti kiholela.

Mwaka jana, alisema kulikuwa na kesi sita za uhujumu uchumi ambazo walizungumza na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), wakalipa faini kubwa kutokana na makosa waliyoyatenda.

Vile vile, alisema kumekuwa na ongezeko la ukataji wa miti kwa mujibu wa taarifa ya mwaka juzi na mwaka huu kiwango ya upotevu wa misitu kimeongezeka.

Alisema mikoa mingi iliyo karibu na miji kutokana changamoto ya ongezeko la mahitaji ya nishati ya kuni na mkaa ikiwamo Mkoa wa Pwani, inakata miti kwa ajili ya nishati hiyo.

"Ni moja ya mikoa ambayo misitu yake mingi haijahifadhiwa, mingi ipo kijijini. Nusu ya misitu yetu ipo katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya ardhi za vijiji hazijahifadhiwa rasmi huko ndiko kunatokea uvunaji ambao hawazingatii sheria kuna wengine wameshikilia kama ni mashamba yao," alisema.

Alisema mtu anaweza kusema anafyeka shamba anataka kufanya kilimo fulani kumbe lengo lake ni kuvuna miti kwa ajili ya shughuli zake.

Silayo alisema kwa miaka ya hivi karibu maeneo ambayo yanatajwa kukata miti kwa wingi ni ambayo mifugo imehamia mikoa ya Kanda ya ziwa ikiwamo Tabora.

Alisema asilimia 92 ya nchi inategemea nishati ya kupikia inayotokana na mimea na asilimia nane inategemea nishati nyingine.

Alisema utegemezi uliopo wa nishati ya kuni na mkaa ni mkubwa kwa sababu hawajapata nishati mbadala ambayo wananchi watamudu gharama, kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nishati na usalama wake kwa ujumla.

"Kuna fikra kwamba nishati mbadala hata kama ikiwapo bado usalama wake ni mdogo ama kuwa na hulka kinachopikwa pale sio kitamu tuwaelimishe wananchi wetu ili kuondoa hiyo fikra na uboreshaji wa maisha ya watu utasaidia kuondokana na ukataji wa misitu kiholela nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Utu na Mazingira (Hudefo), Sarah Pima, alishauri sekta zinazohusika na masuala ya misitu kuweka sheria kali ili kuhakikisha miti haikatwi kiholea ikiwa ni sehemu ya kulinda mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema ukataji wa miti unasababisha athari katika mazingira na mabadiliko ya tabia nchi na hata kuchangia uwapo wa ukame.

Aidha, Pima alisema wakiwa wadau wa mazingira wanaendelea kuelimisha jamii kwa ujumla kufahamu umuhimu wa utunzaji wa miti ili kuithamini.

Alisema wanaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha utunzaji wa mazingira unaendelea kwa manufaa ya nchi ili kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Pima alisema jamii iangalie namna ya kutumia mkaa mbadala ama gesi kwa matumizi ya nyumbani ili kuilinda miti na misitu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tujenge utamaduni kusoma vitabu tuongeze maarifa

**JANA** Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilizindua machapisho manne ya vitabu vinavyotoa miongozo kwa waandishi wa habari namna ya kupata na kutoa taarifa kwa usahihi.

Ingawa kazi kubwa ya Baraza hilo ni kutoa miongozo kwa vyombo vya habari, lakini wananchi pia wanapaswa kutambua haki zao za kupata taarifa zikiwa sahihi na zinazozingatia usawa na weledi kwa kujisomea machapisho mbalimbali yanayoelimisha ili kujiongezea maarifa.

Vitabu vinavyochapishwa na Baraza hilo lengo lake ni kuvikumbusha vyombo vya habari jukumu la kuhabarisha umma kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi bila upendeleo au kumuumiza mtu mwingine.

Kazi ya kuchapisha vitabu hivyo inahusisha mambo mengi, ikiwamo wataalamu, muda na fedha ili kuwapa taarifa muhimu wananchi wa kutambua haki zao za kimsingi.

Baraza la Habari hufanya pia kazi ya upatanishi na usuluhishi inapotokea wadau na wananchi kuandikwa kwenye vyombo vya habari bila kupewa nafasi ya kujieleza na habari hiyo kuwa ya upande mmoja.

Kama wananchi hawatasoma vitabu vinavyozungumzia haki na sheria zinazowalinda, maana yake haki zao zitapotea bure na sifa yao kuharibika.

Wakati vitabu hivyo vikizinduliwa wadau walikumbushwa umuhimu wa pande zote za watoa taarifa, wapelekaji na wapokeaji kufahamu mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa kabla habari haijamfikia msomaji ili isimwathiri mtu yeyote.

Vitabu vilivyozinduliwa ni pamoja na kinachozungumzia jinsi ya kuripoti habari za watoto, ambacho kinakumbusha waandishi kuzingatia weledi na maadili ya uandishi kwa kuandika bila kumwathiri mtoto kwenye maisha yake ya baadaye.

Kitabu kingine kinazungumzia mwongozo wa kupata na kutoa taarifa kwa waandishi wa habari na maofisa habari, ambacho kinakumbusha wajibu wa maofisa habari kutoa ushirikiano kwa vyombo vya habari na kutoa taarifa kwa wakati wanapotakiwa kufanya hivyo ili umma uweze kupata haki ya kupata taarifa.

MCT pia imetoa chapisho linalozungumzia hali ya vyombo vya habari katika kipindi cha mwaka 2020 -2021 na sheria zinazonyima uhuru wa habari na chapisho lingine linahusu mafunzo ya uandishi wa jinsia kwenye vyombo vya habari.

Vitabu hivyo ni mwongozo mzuri utakaoviwezesha vyombo vya habari kuripoti habari zake kwa usahihi bila kuumiza upande wowote.

Wakati vitabu hivyo vikizinduliwa, Rais wa Baraza la Habari Tanzania, Jaji Juxon Mlay, aliwakumbusha waandishi wa habari na jamii kuvisoma vitabu badala ya kuvichukua na kuvifungia kwenye makabati huku wakiacha madini yaliyomo kwenye vitabu hivyo yakipotea bure.

Vitabu hivyo ni msaada tosha vitakavyowaongoza waandishi na wahariri kufanyakazi zao kwa ufanisi na kwa weledi.

Pia aliikumbusha jamii kujenga utamaduni wa kujisomea vitabu ili kupata maarifa na kutambua wajibu wao wanapoona hawajatendewa haki katika kupashwa habari.


Katika ulimwengu huu uliotawaliwa na habari za mitandao ya kijamii, wananchi wengi wamepoteza ari ya kusoma vitabu na kuishia kusoma habari za mitandao ambazo sio zote zenye ukweli kama ilivyo kwenye machapisho ambayo huandika habari za kina.

MCT pia imeshauriwa kusambaza machapisho hayo kwenye vyuo, maktaba, vyumba vya habari, ili watu wengi zaidi waweze kuelimika kupitia madini yaliyomo kwenye machapisho hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kuanzisha nyanda za malisho tiba migogoro wakulima, wafugaji

Na Sabato Kasika

**MAPIGANO** kati ya wakulima na wafugaji, kwenye baadhi ya maeneo ni miongoni mwa migogoro inayoibuka mara kwa mara na licha ya kutafutiwa ufumbuzi bado inajitokeza.

Ipo mifano mingi ya migogoro hiyo ambayo imetokea miaka ya nyuma na kusababisha maafa kwa makundi hayo mawili, lakini mfano mwingine ni wa hivi karibuni katika tukio la Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wafugaji kutoka Arusha wakivamia eneo hilo.

Diwani wa Masama Rundugai (CCM) wilayani humo, Aziz Simbano na wenzake wawili na mwanawe wa kiume, walinusurika kuuawa, baada ya kujeruhiwa na wafugaji waliotaka kulisha kwa nguvu mifugo mazao yake.

Migogoro kama hiyo imekuwa kutokea mara kadhaa katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Pwani, Manyara, lakini baadaye ikawa imetulia baada ya serikali kuingilia kati kuitatua. Lakini kwa tukio hilo la wilayani Hai, ipo haja ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu, ili kuzuia kuiona na kuibuka kama uyoga na kuhatarisha maisha ya makundi hayo mawili.

Binafsi ninadhani njia mojawapo inayoweza kusaidia kupunguza migogoro hiyo, ni kutengwa kwa maeneo ya malisho (nyanda za malisho) na kuyatambua kisheria ili kuzuia uvamizi unaoweza kufanywa na watumiaji wengine wa ardhi.

Iwapo watakuwa na maeneo yao yenye malisho na maji ya kutosha wakati wote, ambayo yanatambuliwa kisheria, ninadhani hawatahama ovyo na kujikuta wakigombana na wakulima kwa tuhuma za kuharibu mazao.

Kwa miaka mingi, Watanzania wamekuwa wakiishi mchanganyiko kuanzia wakulima na jamii ya wafugaji, huku wafugaji wakitumia ufugaji wa asili na kuchangia katika ukuaji wa soko la nyama nchini.

Lakini sasa mtindo wao wa kuhama kutafuta maji na malisho, umekuwa ukichangia kuwapo kwa migogoro kati yao na wakulima ambayo wakati mwingine husababisha mapigano.

> **Kimsingi, wote ni Watanzania, wana haki ya kutumia ardhi kulingana na taratibu zilizowekwa, ndiyo maana ninashauri kutafutwa kwa njia ambayo inaweza kumaliza uhasama huo wa miaka nenda miaka rudi.**

Wakati mwingine mapigano hayo husababisha majeraha na hata vifo kwa makundi hayo na pia kwa mifugo. Hivyo ingekuwa vyema iwapo utashi wa kisiasa utachukua mkondo wake ili kuwa ufumbuzi wa kudumu.

Ninadhani umefika wakati sasa kutumia utashi wa kisiasa kumaliza tofauti za makundi hayo, ili yaishi kwa amani kutokana na ukweli kwamba yote yanategemeana kwa namna moja au nyingine.

Utashi wa kisiasa kwa maana ya viongozi wa kuchaguliwa wenye ushawishi kuingilia kati ili kumaliza tofauti zao, kwani bila utashi wa kisiasa, ninaamini kwamba migogoro na mapigano, vinaweza kuendelea kuibuka. Hatua hizo zinaweza kusaidia kuondoa uhasama kati ya makundi hayo na kuyafanya kuwa na ushirikiano wa kudumu na hata kuendelea na uzalishaji mali ili kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa, mfugaji anaweza kununua mazao kutoka kwa mkulima, na pia mkulima anaweza kununua kitoweo kutoka kwa mfugaji, hivyo suala la ushirikiano wa makundi hayo ni wa muhimu kuliko utengano.

Kimsingi, wote ni Watanzania, wana haki ya kutumia ardhi kulingana na taratibu zilizowekwa, ndiyo maana ninashauri kutafutwa kwa njia ambayo inaweza kumaliza uhasama huo wa miaka nenda miaka rudi.

Siamini katika kuendeleza migogoro, bali njia sahihi za kuimaliza, kwani imekuwa ikisababisha upotevu wa rasilimali kwa raia, jamii na serikali kwa ujumla, uharibifu wa mali, uhai wa raia na mifugo.

Hivyo, ninaona kuna haja kushauri mamlaka husika kila iwezekavyo kuhamasisha suala la amani na ushirikiano kwenye jamii vinahamasishwa, ili kila kundi liendeshe shughuli zake bila chokochoko.

# Muhimbili yatangaza kifo pacha aliyetenganishwa

**Na Romana Mallya**

MMOJA wa pacha waliotenganishwa kwa operesheni maalum katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Neema, amefariki dunia wakati akiendelea na matibabu katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) walikolazwa tangu upasuaji huo ufanyike.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, alisema jana kuwa kifo hicho kilitokea Jumapili na sasa wanaendelea kumtibu pacha aliyebaki, Rehema.

"Ninasikitika kukufahamisha kuwa mtoto Neema ambaye alitenganishwa na mwenzake Rehema, alifariki dunia Julai 10 saa tatu asubuhi.

"Akiwa ICU, hali yake ilibadilika ghafla, madaktari walijitahidi kurudisha hali yake bila mafanikio na hatimaye kupoteza maisha. Tuendelee kumwombea Rehema ambaye bado yupo ICU ili Mwenyezi Mungu amjalie afya njema. Bwana alitoa na Bwana ametoa, jina lake lihimidiwe sana," alisema mkurugenzi huyo katika taarifa yake rasmi jana.

Julai Mosi mwaka huu, jopo la wataalamu 31 wa hospitali hiyo na wengine kutoka nje ya nchi, lilifanikiwa kuwatenganisha watoto hao.

Operesheni ya kuwatenganisha ilichukua saa saba ikihusisha kutenganisha ini, mishipa mikubwa iliyomo humo pamoja na kuitenganisha ngozi iliyopo kwenye moyo.

Neema na Rehema walizaliwa Septemba 21, 2021 kwa njia ya upasuaji wakiwa na uzito wa kilo 4.9 kwa pamoja katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu. Walipewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bugando) na baadaye MNH.

Upasuaji kama huo ni mara ya tatu kufanyika nchini ambapo wa kwanza ulifanyika mwaka 1994, ukihusisha watoto wawili wa kiume waliokuwa wameungana kwenye tumbo.

Upasuaji wa pili ulifanyika mwaka 2018 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi tisa sasa na wanaendelea vizuri.




Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga, wakisaini mkataba wa kuuhisha ushirikiano, katika shughuli mbalimbali kuanzia mwaka huu hadi 2024, wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 1.7 katika ofisi za kituo hicho, Kijitonyama Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasisitiza uamuzi kuwapa nafasi wanafunzi wanaopata ujauzito

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imesema itaendelea kuhakikisha wanafunzi wote waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mimba, wanaendelea na masomo na kupata elimu ili watimize ndoto zao.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitoa kauli hiyo juzi baada ya kutembelea Shule ya Upili Tuliani iliyoko Magomeni, akifuatana na viongozi mbalimbali kutoka wizara hiyo pamoja na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Dk. Victoria Kwakwa.

Katika ziara hiyo, Prof. Mkenda alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha watoto wote waliokatisha masomo, wanarudi shuleni kuendelea na masomo yao.

"Kauli ya Mheshimiwa Rais ni kwamba watoto wote waliokatisha masomo, warudi shuleni ili watimize ndoto zao. Kwa hiyo, hata watoto wa kiume ambao ni watoro, mpango huo upo na unaendelea tutahakikisha watoto wote waliokosa elimu wanapata elimu.

"Kwa hiyo benki hii ya dunia imekuwa ikitusaidia mambo mengi ikiwamo kufadhili wanafunzi kupata elimu hasa wale waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwapo pia masuala ya kifedha," alisema.

Aliwataka wanafunzi waliorejea shuleni, watumie fursa hiyo iliyotolewa na serikali, kusoma kwa bidii ili watimize malengo yao.

"Nimesikia kwa wanafunzi wengine wana malengo makubwa, nilipokuwa nikiongea nao, wapo waliosema wanataka kuwa madaktari bingwa, wapo waliosema wanataka kuwa marubani, wapo waliosema wanataka kuwa walimu, lakini niwaambie nyie wanafunzi siri kubwa ya kufanikiwa hapo ni kusoma kwa bidii," alisema.

Makamu wa Rais wa WB Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Victoria Kwakwa, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia na kupigania watoto waliokatisha masomo, wanarudi shule kutimiza ndoto zao.

"Kwanza nimefurahi kukutana na wanafunzi ambao waliacha shule kwa matatizo mbalimbali wakiwa katika hali ya furaha, lakini wameniahidi kutimiza ndoto zao wakimaliza masomo yao.

"Kwa hiyo, sisi Benki ya Dunia kupitia mradi wa kuimarisha ubora wa elimu katika shule za upili (SEQUIP), tutaendelea kuwaunga mkono mpaka pale watakapotimiza malengo yao," aliahidi.

Mwanafunzi aliyerejea shuleni hapo kwa baada ya kukatisha masomo kutokana na kupata ujauzito shuleni, Rehema Khamisi, alimshukuru Rais Samia kwa kuwapa kibali cha kurudi shuleni kuendelea na masomo.

"Nilipata mimba nikiwa kidato cha nne, nikashindwa kumaliza shule. Kwa hiyo, nimekuja tena, ninasoma madarasa mawili kwa mwaka mmoja (QT), ili nipiganie nitimize ndoto zangu," alisema.

Mwanafunzi huyo mwenye ndoto ya kuja kuwa daktari bingwa wa watoto, aliiomba serikali kuwawekea mazingira mazuri ya kulea watoto wao pindi wanapokuwa shuleni.

## Elimu utunzaji mazingira yawakuna maaskofu

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepongezwa kwa kutoa elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa maaskofu wa Katoliki Afrika Mashariki na Kati.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alipotembelea banda la NEMC lililoko kwenye maonyesho ya kimataifa ya mazingira katika Mkutano wa Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu hao (AMECEA) unaofanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema NEMC imekuwa ikisimamia Sheria za Usimamizi wa Mazingira na kuwaomba wadau kuzingatia sheria hizo ili kulinda mazingira ya nchi.

"Niishukuru taasisi yetu ya NEMC ule usimamizi wa sheria wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana nchini kwetu, kwa hiyo niwaombe sana wadau kushirikiana na taasisi zetu kwenye masuala ya mazingira, watambue wanapotimiza majukumu yao wanataka nchi iwe salama wakati wote.

"Mkutano huu umekuja na ajenda mahsusi ya mazingira ili kuhakikisha yanatunzwa na kuchochea maendeleo endelevu ya dunia. Katika hili, tumshukuru Rais Samia kwa maelekezo ambayo yanaonyesha namna Tanzania ilivyojizatiti kulinda mazingira tukiongozwa na Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021," alisema.

Dk. Jafo alisema ajenda ya mazingira ni mtambuka na sasa kumekuwapo na vikwazo vingi vya kimazingira.

"Tumeshuhudia maeneo mengi sana kiwango cha bahari kinaongezeka, hali ya joto inaongezeka, ukame unashamiri kwenye baadhi ya maeneo hivyo tuna kila sababu ya kutunza mazingira.

"Wananchi wa Tanzania lazima tujali mazingira yetu, tukiharibu mazingira hatuna mahala pa kukimbilia, katika nchi yetu tuna kila sababu ya kulinda, tumeona Jiji la Dar es Salaam limetolewa mfano kwa kuwa jiji bora kwa kuzingatia usafi, miongoni mwa majiji sita Afrika."

Askofu wa Jimbo la Geita, Flavian Kassala, alisema kazi inayofanywa na NEMC kuhusisana na mazingira ni muhimu kwa kuwa imerahisisha uzingatiaji na ufuatiliaji wa sheria za mazingira.

"Hii elimu ni muhimu kuzingatiwa kwani ndiyo msingi imara wa upangaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuzingatia athari zinazoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Akitoa elimu kwa washiriki wa mkutano huo, mtaalamu kutoka NEMC, Suzan Chawe, alisema mabadiliko ya tabianchi yanaathiri miradi ya maendeleo, hivyo ni muhimu kufanya tathmini ya athari za mazingira ili kukabiliana na mabadiliko hayo.

# CRDB, IFC kuongeza upatikanaji mitaji kwa wajasiriamali nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB na Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) jana waliingia mkataba wa uwezeshaji utakaoongeza upatikanaji wa fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati Tanzania na Burundi, na kusaidia kuimarisha uchumi wa nchi zote mbili kutokana na athari za janga la UVIKO-19.

Hafla hiyo ilifanyika katika Hoteli ya Johari Rotana iliyoko katikati ya Jiji la Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi wa taasisi hizo.

Chini ya ushirikiano huo, IFC inatoa mkopo wa dola milioni 100 kwa CRDB Tanzania, nusu ya fedha hizo zitakuwa kwa shilingi za kitanzania na mkopo wa dola milioni tano kwa CRDB Burundi kusaidia mikopo kwa wafanyabiashara wadogo katika nchi zote mbili, hasa kwa biashara zinazomilikiwa na wanawake.

Katika mkataba huo, asilimia 25 ya mkopo unaoelekezwa Tanzania, utatolewa kwa biashara zinazomilikiwa na wanawake. Ilibainishwa kuwa fedha hizo zitaongeza upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu, ambayo imekuwa adimu kupatikana tangu kuzuka kwa janga la UVIKO-19.

Mikopo hiyo ni sehemu ya mpango wa IFC wa uwezeshaji wa tabaka la chini katika uchumi, ambao unalenga kusaidia taasisi za kifedha kutoa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo ambao wameathiriwa zaidi na janga la UVIKO-19. Ufadhili wa IFC pia unasaidiwa na Dirisha la Sekta ya Binafsi la Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa.

Wajasiriamali ni kundi muhimu kwa uchumi wa Tanzania na Burundi. Kwa Tanzania, wastani wa biashara ndogo na za kati milioni 3.2 huchangia asilimia 27 ya Pato la Taifa na kuajiri zaidi ya watu milioni tano.

Hata hivyo, takriban asilimia 81 ya biashara hizo hazina uwezo wa kupata mikopo. Kwa Burundi, biashara pia zinakabiliwa na shida kubwa katika kupata mikopo.

"Fedha hizi zimekuja wakati mwafaka na zitaongeza uwezo wetu wa kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati huku tukisaidia kuongeza usawa wa kijinsia katika mnyororo wa thamani.

"Benki ya CRDB tunaamini kuwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ni msingi wa maendeleo. Wanawake wameathirika kwa kiasi kikubwa sana janga la UVIKO-19, ambalo limepelekea changamoto nyingi za kiuchumi na kuathiri moja kwa moja maisha ya familia na jamii zao," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB wakati wa hafla ya utiaji saini.

Nsekela aliongezea kuwa ufadhili wa IFC utasaidia maendeleo ya sekta mbalimbali za maendeleo nchini, ikiwamo biashara, kilimo, afya, elimu, makazi na miundombinu.

Aliyataja maeneo mengine ni pamoja na miradi inayozingatia mabadiliko ya tabianchi, wajasiriamali pamoja na biashara zinazomilikiwa na wanawake kama ambavyo imesisitizwa katika mkataba huo wa ushirikiano baina ya CRDB na IFC.

"Ushirikiano kati ya IFC na CRDB utasaidia ukuaji wa sekta ya ujasiriamali katika nchi hizi ambapo mchango wao katika ajira na shughuli za kiuchumi ni mkubwa.

"Ushirikiano huu pia unajumuisha jitihada maalum katika kusaidia biashara zinazomilikiwa na wanawake na kuendeleza ushirikishwaji wa kijinsia, ikiwa ni sehemu muhimu ya mkakati wa IFC nchini Tanzania na Afrika," alibainisha Sérgio Pimenta, Makamu wa Rais wa IFC Afrika.

IFC ina uhusiano wa muda mrefu na CRDB. Mkataba huo wa makubaliano wa uwezeshaji kibiashara uliotiwa saini jana, ni wa tano baina ya taasisi hizo, na ni sehemu ya kazi za IFC nchini kusaidia ukuaji wa biashara ndogo na kukuza uwezeshaji kwa biashara zinazomilikiwa na wanawake.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto) na Makamu wa Rais wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) Afrika, Sergio Pimenta (kulia), wakitia saini mkataba wa makubaliano ya mkopo wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 105 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali nchini, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yalia na barabara, stakabadhi ghalani

**Na Mwandishi Wetu,** KILWA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuchukua hatua kukabiliana na kero za ubovu wa miundombinu ya barabara, uhaba wa maji na mfumo mbovu wa soko la mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye Jimbo la Kilwa Kusini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu Ado, kwenye ziara yake ya kata kwa kata inayoendelea katika Jimbo la Kilwa Kusini mkoani Lindi.

Hadi jana, Ado alikuwa ameshatembelea Kata za Masoko, Kikole, Likawage, Nanjilinji, Kiranjeranje na Lihimalyao.

Akiwa Kata ya Nanjilinji, Ado aliitaka serikali kuchukua hatua kuifanyia ukarabati barabara ya Ngea/Likawage hadi Nanjilinji kwa kiwango cha Changarawe na kujenga barabara ya Kiranjeranje/Nanjilinji hadi Ruangwa kwa kiwango cha lami.

"Nimesafiri usiku kutoka Likawage hadi Nanjilinji. Nimesikitika sana. Sijawahi kuona njia mbovu kama hiyo. Hakuna atakayeamini kuwa njia hiyo ndiyo njia inayoelekea katika eneo linalozalisha ufuta bora zaidi nchini na kuingiza ushuru wa zaidi ya Sh. milioni 600 kwa mwaka. Hili halikubaliki," alisema.

Akiwa katika Kata ya Lihimalyao, Katibu Mkuu aliitaka serikali kuchukua hatua za haraka kukabiliana na uhaba mkubwa wa maji unaotikisa huko.

"Serikali isikie. Watu wa Lihimalyao wanaishi kwa shida kubwa kwa sababu ya maji. Watu wanashindwa kuoga na maji ya kunywa ni machungu. Ndugu yangu Juma Aweso, Waziri wa Maji, kama tuliweza kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mikoa mbalimbali, tunashindwa kuvuta maji kutoka Mikoma kwenda Lihimalyao?" Ado alihoji. Mbali na hayo, akiwa kwenye kata zote alizotembelea, Katibu Mkuu alipokea kero za wakulima wa ufuta na korosho hasa kuhusu kile alichokiita kufeli kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kuwapatia wakulima soko la uhakika la mazao.

"ACT-Wazalendo imesikia kilio cha wakulima wa korosho na ufuta. Mmesema wazi kuwa hamuitaki stakabadhi ghalani kwa sababu hamlipwi vizuri na kwa wakati. Bila shaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, atazipata salamu zenu. Kama hawawezi kuzikabili changamoto za stakabadhi ghalani, bora kurejesha soko la ushindani," alisema Ado.

Jana Ado atafanya ziara kwenye Kata za Pande na Mandawa. Ziara ya Katibu Mkuu inahitimishwa leo kwa kufanya kikao na wanachama kwenye Kata ya Kivinje. Kwenye ziara hiyo, Katibu Mkuu ameambatana na Katibu wa Sera na Utafiti, Idrisa Kweweta, na viongozi wa Mkoa wa Lindi na Jimbo la Kilwa Kusini.

## Ujenzi gati waongeza mapato ya Bandari

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

SERIKALI imebainisha kuwa kujengwa kwa gati jipya katika Bandari ya Mtwara kumeongeza mapato yanayokusanywa katika bandari hiyo kutoka Sh. bilioni 14 mwaka 2020 na kufikia Sh. bilioni 23 mwaka 2022.

Akizungumza baada ya kutembelea bandari hiyo jana, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema kukua kwa mapato hayo kumechangiwa na maboresho yaliyofanywa katika bandari hiyo kwa kuongeza gati nyingine kubwa yenye uwezo wa kuhudumia meli yenye uwezo wa kubeba tani 65,000.

"Serikali imewekeza hapa na ndiyo maana tunaona matokeo ya kupanda kwa mapato lakini hii isiishie hapa, tunahitaji mapato zaidi kwani mzigo wa kupitisha hapa upo wa kutosha ambapo kama tutajipanga vizuri, basi tunaweza kukusanya zaidi," aliagiza.

Naibu Waziri Mwakibete alieleza umuhimu wa kuitangaza zaidi bandari hiyo na kusema kuwa bila kuitangaza bandari hiyo, kampuni kubwa kama za simenti, makaa ya mawe, korosho zinaweza kuendelea kutumia barabara badala ya kutumia bandari.

Aliitaka Mamlaka ya Bandari (TPA) kuitisha vikao vya mara kwa mara vitakavyowakutanisha wadau wote wa usafiri na usafirishaji ili kujadili namna nzuri ya kutumia bandari hiyo ambayo imeboreshwa kwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 150.

Meneja wa Bandari ya Mtwara, Abdilah Salim, alimhakikishia Naibu Waziri Mwakibete kuwa TPA iko kwenye mpango wa kutenga maeneo kwa wafanyabiashara wakubwa kama Dangote anayesafirisha simenti na Kampuni ya Ruvuma ambayo inasafirisha makaa ya mawe na wasafirishaji wa korosho ili kuhakikisha wanasafirisha mizigo yao kwa wakati bila vikwazo vyovyote.

Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano, Thomas Mushi, alisema tayari juhudi mbalimbali zimeanza kufanyika kwa kuitangaza bandari hiyo ndani na nje ya nchi ili kuwavutia wasafirishaji wengi hususani wa nchi za Zambia na Malawi ambao wanatumia Bandari ya Dar es Salaam.

Naibu Waziri Mwakibete yuko mkoani Mtwara kwa ziara ya siku mbili ya kukagua miundombinu inayosimamiwa na taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo.

## DC aonya vishoka uunganishaji maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewaonya wananchi kutumia mafundi wa mitaani kwa ajili ya kuwaunganishia maji kwa kuwa baadhi yao wanatumia nafasi hiyo kufanya hujuma katika miradi mbalimbali.

Alitoa onyo hilo juzi wakati akikagua ujenzi wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Manispaa ya Shinyanga ambayo imetekelezwa kwa fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Shinyanga (SHUWASA).

Alisema baada ya kuitembelea miradi ya maji ambayo yote imekamilika na kuanza kutoa huduma ya maji safi na salama, amewataka wananchi watume maombi SHUWASA ili waunganishiwe huduma hiyo majumbani mwao.

"Tunampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea fedha hizi za UVIKO-19, na kutatua kilio cha wananchi cha muda mrefu waliokuwa wanahitaji huduma ya majisafi na salama na miradi imekamilika, hivyo ninawasihi wananchi muitunze miundombinu ya miradi hii ya maji msiihujumu.

"Tumeni maombi SHUWASA, ili waje wawaunganishieni maji majumbani mwenu na msije mkajaribu kujiunganishia kinyemela, mtaharibu mabomba na atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali," alionya.

Katika hatua nyingine, mkuu wa wilaya huyo aliipongeza SHUWASA kwa kutekeleza miradi hiyo ya maji kupitia fedha za UVIKO-19 kwa wakati na kiwango kinachotakiwa.

Alisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo, zimebaki na kwamba zitatumika kupanua mtandao wa maji katika maeneo mengine.

Mkurugenzi wa SHUWASA, Yusuph Katopola, alisema walipokea fedha za UVIKO-19 Sh. milioni 469 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na wametumia Sh. milioni 406.

Alisema miradi hiyo ya maji walielekeza kwenye maeneo ambayo hapakuwa na huduma hiyo vikiwamo vijiji vya Magwata, Bugwandege, Bugimbagu, Didia pamoja na Iselamagazi.

Baadhi ya wananchi ambao wamepata huduma hiyo ya maji akiwamo, Ashura Masanja, mkazi wa Magwata, walisema kwa sasa wameondokana na shida ya kutumia maji yasiyofaa.

Alisema kabla ya kupatikana kwa huduma hiyo, walikuwa wanatumia maji ambayo mifugo ilikuwa ikinywa, hivyo kuhatarisha afya zao.

# RAS ashtuka mmomonyoko wa maadili kwa vijana nchini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKOA wa Singida umeanzisha programu maalum ya malezi na makuzi kwa vijana wa kiume wanaosoma katika shule zenye mchepuo wa sayansi ambao watakuwa wanafundishwa mambo mbalimbali yakiwamo masuala ya maadili, nidhamu na stadi za maisha.

Katika programu hiyo ambayo imeasisiwa na Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, mafunzo yake yameanza kutolewa kwa wanafunzi wanaosoma katika shule za Ilongero, Mwenge na Lulumba zilizopo mkoani hapo kwa lengo la kuwapa hamasa zaidi vijana katika masomo yao.

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Maria Lyimo, akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa programu hiyo, alisema itakuwa ni chachu kwa halmashauri zote za mkoa huo kuhakikisha zinakuwa na programu ya aina hiyo kwa wanafunzi waliopo kwenye shule za msingi na sekondari.

Lyimo alisema kuanzishwa kwa programu hiyo ambayo kaulimbiu yake ni 'Mwili Wangu Maisha Yangu', itawasaidia na kuwajengea uwezo vijana kuhusiana na stadi za maisha na uzalendo na hivyo kuwa chachu na hamasa kwao wanapokuwa shuleni na hata wanapohitimu masomo na kurejea majumbani.

Mshauri wa wanafunzi kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania Mkoa wa Singida, Ambwene Kajula, alisema katika ulimwengu wa kidigitali, maadili yamepungua, tabia za watoto zinabadilika na utandawazi unapotosha misingi kamili ya nchi.

Kajula alisema kuanzishwa kwa programu hiyo kutawasaidia vijana kulinda miili yao na kuwa na maadili mema kwa kutojiingiza katika vitendo vya uhalifu ambavyo haviendani na maadili ya Kitanzania.

"Nidhamu ya leo ndiyo inajenga Taifa bora la kesho, ndiyo inayojenga kupata maendeleo mazuri ambayo unayataka, huwezi ukawa mwanasayansi mzuri kama hujui kutunza muda, fedha na kuhakikisha mwili wako unakuwa na afya njema," alisema.

Mratibu wa Ukimwi Mkoa wa Singida, Lewis Rwegayula, alisema vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 25, bado ni kundi kubwa ambalo linapata maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Alisema kupitia programu hiyo, vijana sasa watapewa elimu ya namna ya kukabiliana na janga la Ukimwi na hivyo kusaidia kupunguza maambukizi mapya ambapo kwa Mkoa wa Singida kiwango cha maambukizi ni asilimia 3.6.

"Tunamshukru RAS (Katibu Tawala Mkoa) kwa kubuni suala hili na kwa maelezo yake litakuwa la kudumu na litafanyika kwa vijana wa kike pia na matarajio ni kufikia shule za msingi na sekondari zilizopo mkoa wa Singida," alisema.

Wakati wa kongamano hilo, wanafunzi walipewa mada kadhaa ikiwamo nidhamu na maadili, uzalendo, Ukimwi na vijana, pia kulikuwa na mashindano ya kuimba, mashindano ya ngoma za kiutamaduni, wasilisho la michoro ambapo washindi walipewa zawadi.




Balozi wa Biko Tanzania, Kajala Masanja (kushoto), akimkabidhi fedha zake Rashid Ally, Sh. milioni 10 alizoshinda kutoka kwenye droo kubwa iliyochezeshwa mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB Tawi la Palm Beach, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA na mitandao ya simu wakutana kuboresha huduma

**Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na watoa huduma za mawasiliano ya simu nchini wamekutana kujadili mpango wa kuboresha huduma za mawasiliano ya simu hasa katika maeneo ambayo ufikishwaji wa huduma hiyo haujafikia viwango stahiki vya ubora.

Kikao hicho kilichofanyika kwenye Ofisi za Makao Makuu ya TCRA jana mkoani Dar es Salaam kiliwakutanisha Vodacom Tanzania, Mic Tanzania (Tigo), Aitel, TTCL na Halotel na maofisa wa Idara ya Leseni na Ufuatiliaji wa TCRA.

Hoja zilizojadiliwa na pande hizo mbili ni namna watoa huduma wanavyoweza kufanyia kazi kwa kurekebisha kasoro za huduma katika maeneo yaliyoainishwa ambapo TCRA mara baada ya kupokea mpango kazi wa watoa huduma itafanya upimaji kwa mara nyingine ili kujiridhisha ikiwa watoa huduma wamefanya maboresho katika maeneo bayana.

Mhandisi Mwandamizi wa TCRA, Mwesiga Barongo, aliyeongoza kikao hicho, alisema pande hizo mbili zimekubaliana masuala kadhaa ambayo yatashuhudia watoa huduma wakitekeleza, kisha kupeleka mrejesho kwa TCRA ikiwa wameboresha huduma hizo.

"Kila mtoa huduma alikuwa na kiwango chake cha matokeo ya upimaji ubora wa huduma; hivyo kwa maeneo yenye upungufu wa ubora tumewaelekeza kwa kuwataka waandae mpango kazi ambao wanapaswa kuutekeleza kwa kuhakikisha maboresho ya huduma kwenye maeneo 15 tuliyopima kote nchini, baada ya hapo TCRA tutapima tena kabla ya mwaka huu kumalizika ili kujiridhisha ikiwa wamefanyia kazi maeneo yaliyobainika kuwa na uduni katika ubora wa huduma," alisema.

Barongo alitaja baadhi ya maeneo ambayo TCRA iliyapima ili kuthibitisha ubora wa huduma nchini kuwa ni pamoja na Unguja, Pemba, Kyela, Mpanda, Dodoma, Nkasi, Sumbawanga, Moshi, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Kinondoni, Ilala, Tabora na Tanga na kwamba baadhi ya watoa huduma walibainika kuwa na kiwango duni cha utoaji huduma ambapo wamepewa maelekezo kuhakikisha wanapandisha kiwango cha ubora wa huduma.

Katika kikao hicho, TCRA iliwaelekeza watoa huduma kuhakikisha wanafanya marekebisho hayo kwa muda mfupi kadri iwezekanavyo na ikiwa watakabiliwa na vikwazo, hawana budi kuomba usaidizi wa TCRA hasa katika eneo la upitishaji miundombinu ya mawasiliano.

Watoa huduma walipata fursa ya kutoa ufafanuzi wa namna watakavyoboresha huduma katika maeneo mbalimbali ya nchi yaliyoainishwa ambayo yalibainika kuwa na kero za huduma kupitia chati ya upimaji wa ubora wa huduma ambayo kwenye kikao hicho, TCRA kwa pamoja na watoa huduma waliipitia na kukubaliana namna mtoa huduma husika atakavyoboresha huduma.

Wakizungumza pembezoni mwa kikao hicho, watoa huduma hao kwa nyakati tofauti waliahidi kufanyia kazi maelekezo ya uboreshaji wa huduma.

TCRA hufanya upimaji wa ubora wa huduma kwa watoa huduma za mawasiliano kila robo mwaka kisha hutoa taarifa ya upimaji ambayo hulinganishwa na upimaji unaofanywa na watoa huduma ambapo mara baada ya taarifa za pande zote mbili kuletwa pamoja, maafikiano ya kitaalamu hufikiwa kisha TCRA hutoa maelekezo kwa watoa huduma kufanya maboresho kwa maeneo ya huduma yaliyobainika kuwa na kasoro.

# Balozi kodi ahamasisha wananchi ulipaji wa kodi

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

BALOZI wa Kodi amewataja wananchi kulipa kodi kwa hiari ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutimiza lengo lake la kukusanya Sh. trilioni 23 katika mwaka wa fedha wa 2022/23.

Subira Mugalu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), alitoa rai hiyo jana katika Banda la TRA kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba.

Alisema kiwango hicho ambacho TRA inatarajia kukikusanya, ni sehemu ya Sh. trilioni 41.48 ambazo serikali inatarajia kukusanya katika mwaka mpya wa fedha.

"Kwenye mwaka wa fedha ulioisha Juni 30, mwaka huu (2021/22), TRA ilikusanya zaidi ya trilioni 22.28, ikiwa ni asilimia 99 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 22.48, tumeanza mwaka wa fedha mpya ambao serikali inatarajia kukusanya Sh. trilioni 41.48 na katika kiwango hicho, TRA imekasimiwa kukusanya Sh. trilioni 23," alisema Subira.

"Kupitia ushirikiano wetu Watanzania na namna ambavyo tutakuwa tumeiva kwa elimu ya kodi ambayo tumeipata kwenye maonyesho haya, tuna uhakika mamlaka hii itavuka lengo," alihimiza.

Subira alisema katika maonyesho hayo ya 46, idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza kupatiwa elimu ya kodi, wakiwamo wawekezaji kutoka nje ya Tanzania.

"Idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza kupatiwa elimu ya kodi na kipekee kabisa ni kwamba hata wawekezaji wamejitokeza kupata elimu ya masuala ya kodi ya nchi yetu na inaonyesha baada ya maelezo mbalimbali, wamevutiwa kuwekeza nchini.

"Kwa hiyo, wote waliotembelea banda hili, wamepata elimu mahsusi katika kampeni inayoendelea ya kutoa risiti na kudai risiti," alisema.

Aliongeza kuwa elimu nyingine ambayo TRA imeitoa kwa wananchi waliotembelea katika maonyesho hayo, ni namna ya kutoa taarifa pale wanapowabaini maofisa wasiowaaminifu wanaoshughulika na ukusanyaji wa kodi hiyo.

"Katika banda hili, kulikuwapo pia kitengo cha maadili ambacho kinatoa fursa kwa Watanzania wenzetu pale wanapoona mwenendo usiofaa kwa maofisa wanaoshughulika na masuala ya kukusanya kodi, kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili washughulikiwe kisheria,"alisema.

Balozi huyo pia alisema TRA imejipanga kuongeza zaidi wigo wa walipakodi kwa lengo la kukusanya zaidi mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Aliwataka Watanzania kutii sheria bila shuruti kwa kulipa kodi na kudai risiti kwa kila ununuzi wanaofanya huku akiwataka wafanyabiashara kuwaamini kwa kutoa risiti hizo.

"Ninaamini tukishirikiana kwenye elimu hiyo na tukatekeleza, tutaiwezesha serikali kufanikisha malengo yake ya kutekeleza mipango ya maendeleo," alisema.

Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa TRA, Peter Shewiyo, alisema katika maonyesho hayo wametembelewa na idadi kubwa ya watu, wakiwamo kutoka nje ya Tanzania ambao walitaka kufahamu elimu ya kodi ya Tanzania na namna misamaha ya kodi inavyopatikana kwa waowekeza.

"Kwa hiyo, katika Sabasaba hii tumepata ugeni mkubwa sana na kila aliyefika, tumempatia elimu na kuonyesha kuridhika," Shewiyo alisema.




Ofisa Masoko na Mauzo wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipment's Ltd, Poul Msuku, akielezea ubora wa magari ya mizigo (Trucks) ya FAW kwa baadhi ya wateja waliotembelea banda lao kwenye viwanja vya Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuiwezesha TPDC

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema serikali itaendelea kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili liendelee kutekeleza kwa ufanisi mipango yake.

Akizungumza katika banda la TPDC kwenye maonyesho ya Sabasaba, Makamba alisema anavutiwa na kasi ya uwekaji wa mfumo wa gesi kwenye magari ambao unafanywa na mamlaka hiyo.

"Niwapongeze TPDC mnafanya kazi nzuri, nimevutiwa na kasi mnayoenda nayo ya uwekaji wa mfumo wa gesi asilia kwenye magari, endeleeni hivyo hivyo," January alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wanaotembelea maonyesho hayo yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba, kwenda kujifunza namna ya kuweka mfumo huo wa gesi katika magari yao.

Kwa mujibu wa TPDC, kuna kiwango cha gesi hiyo asilia cha futi za ujazo trilioni 57.54 ambacho kimegundulika.

# Nape ataka jengo la kudumu TCRA viwanja Sabasaba

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ameiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwa na jengo la kudumu katika Viwanja vya Sabasaba ili iwe huru kutoa huduma ya uhakika kwa wananchi wanaotembelea maonyesho hayo.

Nape alitoa agizo hilo alipotembelea banda la mamlaka hiyo na kutoridhishwa na ufinyu wa nafasi katika banda hilo.

Alisema TCRA ni mamlaka kubwa na ina uwanda mpana katika kuhudumia Watanzania na maonyesho hayo ni sehemu maalum na muhimu ambako wananchi wanapata fursa ya kipekee kwenda kujifunza na kuhudumiwa.

Alisema ni vyema mamlaka hiyo ikawa na jengo lake la kudumu ambalo italitumia kila mwaka.

"Kwa kweli nimekuja kwenye hili banda la TCRA, sijaridhishwa na hili banda lililopo kwa sababu ni finyu sana tofauti na ukubwa wa mamlaka," alisema Nape.

"Mbali na hilo, pia haipendezi kuona kila mwaka inahama, mwaka huu wako hapa na mwaka mwingine wamehamia kwingine, hii inawachanganya wananchi ambao wanakuja kuhudumiwa.

"Si hilo tu, hii mamlaka ina uwanda mpana wa kutoa huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, inapotokea wamekuja kwa wingi kwa pamoja wakajaa humu na hili joto inaleta shida namna ya kuwahudumia," alisema.

Nape alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa Watanzania kujenga tabia ya kutumia maonyesho hayo kwenda kujifunza shughuli mbalimbali zinazotolewa na TCRA.

## UCHAGUZI CCM:
## Vigogo walioibuka baada ya ukimya wanavyochambuliwa

Ukurasa 12



Ukurasa 14



## YALIYOMFIKA BORIS JOHNSON

siasa
JUMATANO JULAI 13, 2022
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

### MIAKA 21 BILA MAKAMU WA RAIS DK. OMAR ALI JUMA

# Mshumaa wa SMZ unaodumu kung'ara kuvuka mipaka ya Muungano ilikogota

### •Mzee Ali Ameir: Namjua, bosi wangu, pia nilimkubali sana

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

WIKI ya Sabasaba inafikia ukingoni ikibeba bashasha, furaha na tabasamu ya hadhira ndani yake, kwa maana ya kuwa bidhaa ya kitaifa. Lakini, ikirejewa miaka 21 iliyopita, mwaka wa sherehe hiyo ilibeba mchanganyiko wa huzuni.

Hiyo ni kwa maana ya kiongozi wa juu kitaifa, Makamu wa Rais, Dk. Omar Ali Juma, aliuaga umma wa Watanzania kwa kutembelea Viwanja vya Maonyesho vya Sabasaba, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa Julai 4 mwaka 2021, moja ya vibanda alivyovitembelea Dk. Omar, ni 'zoo' za wanyama eneo ambalo lilikuwa taaluma yake alikobobea, udaktari wa wanyama.

Marehemu Dk. Omar, baada ya kutembelea viwanja hivyo alirejea jioni kwake, Oysterbay Dar es Salaam, nyumbani alimokuwa na faragha, pia mjumuiko wa kirafiki na busara akiwa na wanawe aliowaasa mema, ikiwamo kukazia masomo kwamba ndio ufunguo wa maisha, hata yeye umemfikisha alikokuwa .

Usiku huohuo muda mfupi baada ya kwenda kitandani, ya Mola yakatimia, nchi ikazama katika simanzi Julai 5 ikiwa ndani ya msiba na maombolezo, ambayo mazishi yakahitimishwa na maziko kijijini Wawi Pemba, kisiwani: alikozaliwa Juni 26 mwaka 1941, eneo la Chake Chake.

Hapo, mwanafunzi wa Shule ya Msingi, Lusinde, iliyopo wilayani Chamwino ,mkoani Dodoma, ambaye leo hii ni mtu mzima ofisini, ana kumbukumbu yake namna walivyogongewa kengele muda wa asubuhi kujuzwa msiba uliolifika Taifa, hapo ukawa mtawanyiko wa kila mmoja kurudi nyumbani, mbwembwe za kuruka ruka kiutoto zilipoa, nao wakiwa kwenye huzuni japo hawakujua kwa undani.



Dk. Omar Ali Juma, alipokuwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar, akimsabahi kiungo wa timu ya soka ya taifa -Taifa Stars, Hussein Amaan Marsha (kulia), kabla ya mchezo wa kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, dhidi ya Uganda Septemba 3, 1994 katika Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

Ufafanuzi wa kilichojiri katika tukio hilo kwa mzaliwa huyo wa mkoa wa Kusini Pemba, ulitokana na andiko la siku chache baadaye, kutoka kwa aliyekuwa mwanahabari wa ofisini kwake, Said Ameir.

Kwa mujibu wa Said Ameir, hadi jioni hiyo ya tukio, alikuwamo katika mjumuiko huo, akapatiwa taarifa mbaya saa chache baada ya yeye kuaga mahali hapo,

hali iliyomlazimisha ageuze haraka kutoka kwake, ambako hapakuwa mbali sana. Kwa ujumla, ni simulizi iliyotimiza neno la Muumba kwa maisha ya mwanadamu.

Hata kiutawala nchini, huenda kupitia hilo likawa moja kati ya mitihani migumu iliyowahi kumkuta na kumuumiza Rais wa Awamu ya Tatu Benjamin Mkapa, kufiwa na makamu wake.

Itakumbukwa kuwa Dk. Omar alibeba wasifu wa kuwa imara katika majukumu yake, huku akitajwa hakuwa na makuu, hali iliyowafanya Watanzania kuwa katika pigo la kumpoteza kiongozi shupavu, mzalendo na muumini wa Muungano, aliyethamini umoja kwa hali na mali.

Kuna sifa ambayo anaendelea kuwa nayo hasa Zanzibar, penye mzizi wake wa asili, kwamba hakuwa na 'mkono wa birika' ana hulka ya ukarimu wake katika utawala.

Wanamuelezea katika maisha yake alipenda sana kuwasaidia watu mbalimbali, anaowajua na asiowafahamu, akisikiliza shida na matatizo kwenye jamii, yu mzungumzaji, mcheshi, mpenda mzaha na masihara yasiyopitiliza.

**WALIOMJUA WAELEZA**

Kabla ya kuwa Makamu wa Rais, Dk Omar amekuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), iliyokuwa chini ya Rais, Dk. Salmini Amour.

Awali aliongoza serikali katika nyadhifa kadhaa, ikiwamo Katibu Mkuu katika Wizara ya Kilimo katika SMZ kuanzia Januari 25 hadi 1988, kisha akateuliwa kuwa Waziri Kiongozi kuanzia Januari mwaka 1988 hadi Oktoba mwaka 1995.

Kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2001, mwanasiasa huyo alihudumu katika nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Urais wakati huo, Benjamin Mkapa, aliposhinda uchaguzi.

Dk. Omar atakumbukwa kuwa ni mwana - CCM aliyeng'ara kisiasa kuanzia kwa Visiwani, Pemba wakati huo kukijulikana kuwa mhimili mkuu wa chama cha upinzani - CUF, chini ya kinara wake, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa mgombea urais wake.

Kimsingi, uliporudishwa mfumo wa vyama vingi kisheria mwaka 1992, Zanzibar chini ya Rais Dk Salmin Amour, ushindani kati ya CCM na CUF, ulikuwa juu kulinganishwa na mtifuano wa kisoka Zanzibar, baina ya mashabiki wa Small Simba na Malindi.

Kulitawaliwa staili ya ushindani, ungwe moja mathalani kukawepo mkutano wa hadhara wa CUF kwenye viwanja vya Malindi Unguja na mgeni rasmi akawa Katibu Mkuu wa CUF, Shaaban Khamisi Mloo, basi siku iliyofuata si ajabu CCM wanaitisha mikutano, kujibu mapigo, mgeni rasmi akiwa Naibu Katibu wa CCM - Zanzibar, Mzee Ali Ameir Muhammed.

Palipotokea mkutano wa CUF kuhutubiwa na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wakati huo, Maalim Seif Sharif Hamad, kesho yake CCM wanapanda jukwaani vyuma kama si ajabu Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar Dk. Salmin Amour, anakwea kuhutubia.

Katika ulingo huo wa siasa, Dk. Omar, akishuhudiwa si mtu wa kusubiri kuhutubia mikutano ya hadhara Unguja au Pemba, badala yake alisafiri hadi mikoa yote ya Tanzania Bara wakati wote.

Mzee Ali Ameir, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika Serikali ya Muungano, na Dk. Omar, na kabla ya hapo kuwa Mhariri Mtendaji wa Shirika la Magazeti ya Chama (SMC), sasa Uhuru Publications alikotumikia tangu ujana, anasema anamfahamu fika, kwa sababu alikuwa bosi wake kwenye Baraza la Mawaziri.

Anasema, pia kuwa alirithi kazi ya Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, kutoka kwa Dk. Omar, wakati huo akishikilia wadhifa wa Waziri Kiongozi wa SMZ, akimsifu alikuwa kiongozi hodari na shupavu.

Mzee Ali Ameir, anampa sifa ya kuwa mwaminifu na mpenda watu, kwa sababu aliwasikiliza watu mbalimbali bila ya kujali nafasi walizokuwa nazo kiuongozi au kiuchumi na kila aliyefika kwake alimpokea kwa upendo na heshima zote.

"Nikisema hapa nizieleze sifa zake sitazimaliza leo maana Dk. Omar alikuwa kiongozi na mtu wa watu mchapa kazi asiye na majivuno," anaongeza Ali Ameir.

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM - Zanzibar, Vuai Ali Vuai, anamtaja marehemu Dk. Omar, kisiasa ni mwana - CCM kindakindaki, pia mwenye ushawishi mkubwa.

Vuai anasema, wakati Dk. Omar akiwa Waziri Kiongozi, yeye alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Vijana, hivyo alikuwa anaiongoza CCM na serikali, akimpa wasifu wake wa ushupavu katika uongozi, bado anaukumbuka hadi sasa.

"Naweza kusema kuwa tumepoteza kiongozi shupavu na hodari lakini pia mwenye ushawishi mkubwa katika siasa za Zanzibar na Bara, "anahitimisha Vuai.

UCHAGUZI WA CCM

# Vigogo walioibuka baada ya ukimya wanavyotathminiwa



James Lembeli, mbunge wa zamani wa Kahama, ni miongoni mwa wakongwe waliokaa kimya, sasa wameibuka tena. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

JOTO la uchaguzi ndani ya CCM linaendelea kupanda, hasa kutokana na baadhi ya vigogo wa chama hicho kuamua kujitosa kwenye kinyang'anyiro baada ya kupotea kwenye majukwaa ya siasa miaka mitano iliyopita.

Kwa sasa uchaguzi umefikia ngazi ya wilaya na mikoa, ambapo makada wa CCM wanachukua fomu za kuwania uenyekiti wa wilaya, mikoa, halmashauri kuu na mkutano mkuu, ambazo zilianza kutolewa Julai 2 mwaka huu.

Zipo sura za wabunge wa zamani, wenyeviti CCM wa mikoa waliowahi kukitumikia chama lakini baadaye hawakusikika tena, wameibuka upya baada ya ukimya wa zaidi ya miaka mitano.

Ni pamoja na mbunge wa zamani wa Kinondoni, Idd Azzan, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Dar es Salaam, Ramadhan Madabida na Hamis Mgeja aliyekuwa Mwenyekiti Shinyanga na mbunge wa zamani wa Kahama, James Lembeli hao ni miongoni mwa waliojitosa katika uchaguzi huo.

Kutokana na hatua hiyo ya vigogo kurejea kwa kishindo, Nipashe imezungumza na baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa ili kupata maoni yao jinsi wanavyochukulia.

> "Ninaamini kwamba, wanasiasa ambao hawakubaliani na siasa za mrengo wa kulia ndiyo waliamua kujiweka pembeni katika kipindi chote hicho, na sasa wamebaini kuwa siasa za mrengo wao ndizo zilizopo," anasema.

**SIASA NI SANAA**

Mchambuzi wa siasa, Abbas Mwalimu, anasema siasa ni sanaa, na kwamba inategemea mazingira na wakati, na kwamba vigogo wa CCM walioamua kuibuka, wameangalia mazingira na wakati kwamba vinawaruhusu.

"Wamebaini kuwa kiongozi wao anafanya siasa za mrengo wa kushoto, kwa maana kwamba anakubali ushauri, hoja mbadala na anahitaji ushirikishwaji, ambavyo kimsingi ni vitu muhimu katika siasa," anasema Mwalimu.

Anasema, kwa sasa, mtu anayependa siasa ni lazima atajitosa kuwania uongozi, kwa madai kwamba mazingira na wakati vinaruhusu kila mtu kushiriki na kujadili na kukosoa jambo bila woga.

"Ninaamini kwamba, wanasiasa ambao hawakubaliani na siasa za mrengo wa kulia ndiyo waliamua kujiweka pembeni katika kipindi chote hicho, na sasa wamebaini kuwa siasa za mrengo wao ndizo zilizopo," anasema.

> "Kila mtu ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa ili mradi awe na sifa, hivyo kurejea kwa vigogo hao katika siasa ni jambo la kawaida, wamesoma ishara za nyakati na kubaini kuwa wanaendana na siasa za sasa," anasema Mjengwa.

Anafafanua kuwa, katika siasa kuna mambo matatu ya kuzingatia, kama itikadi, falsafa na utu, na kwamba iwapo kiongozi hatayazingatia, wafuasi wake wanaweza kujiweka pembeni.

Inawezekana waliamua kuwa kimya baada ya kuona itikadi ya chama na falsafa yake havizingatiwi, lakini pia suala la utu hivyo wakaona njia bora ni kukaa kimya," anasema.

**MAKADA WAONYA**

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka anasema, kila mwana CCM ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, lakini anatoa onyo kwa wale watakaokwenda kinyume na taratibu, kwamba watachukuliwa hatua.

"Uchaguzi wowote unaofanyika kuna kila aina ya njama, kwa sababu kila mmoja anataka kushinda, hivyo CCM itahakikisha uwanja unakuwa sawa kwa kila anayewania uongozi," anasema Shaka.

Shaka anasema CCM haitaki uchaguzi ambao viongozi wanakuwa na majina yao mfukoni mbali kila mwenye sifa ashiriki katika kuchagua au kuchaguliwa ili kupata viongozi sahihi ambao chama kinawataka.

"Kwa kuzingatia hilo, sehemu ambayo kulikuwa na changamoto za aina hiyo, ugawaji fomu ulirudiwa upya ili kuhakikisha kila kada anayetaka uongozi, ashiriki bila kuwekewa mizengwe," anasema.

Anasema, jambo la msingi ni mtu kuwa na sifa za kuwania uongozi, huku akitoa onyo kwa wanachama wa CCM watakaokwenda kinyume na taratibu na kufafanua kuwa watachukuliwa hatua.

"CCM haibagui makada wale, wawe waliowahi kuwa viongozi na wapya, kila mmoja ana haki, jambo la msingi ni kuwapo kwa uwanja mpana usiobagua ili wana CCM wachague kada wanayemtaka," anasema.

**ISHARA ZA NYAKATI**

Mchambuzi wa siasa, Maggid Mjengwa anasema, wana CCM ambao wameibuka upya baada ya kimya cha muda mrefu, wamesoma ishara za nyakati na kubaini kuwa siasa za sasa zinawafaa.

"Kila mtu ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa ili mradi awe na sifa, hivyo kurejea kwa vigogo hao katika siasa ni jambo la kawaida, wamesoma ishara za nyakati na kubaini kuwa wanaendana na siasa za sasa," anasema Mjengwa.

Anasema kila zama leo kuna maridhiano na hiyo kuvutia wanasiasa wengi kushiriki wakiwamo wale waliokuwa wamejiweka pembeni. "Hata baadhi yao ambao wamechukua fomu, wamekaririwa na vyombo vya habari wakidai kwamba, mazingira rafiki ya siasa ndiyo yamefanya waamue kuchukua fomu, ndiyo maana nikasema kila zama na kitabu chake," anasema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga anasema suala la mtu kufanya siasa au kupumzika ni haki yake ambayo haiingiliwi na mwingine.

"Ninadhani waliamua kupumzika baada ya kubaini kuwa hawawezi kuendana na siasa zilizopita, na sasa wameona wanaweza kuendana na siasa zilizopo, hiyo ni haki yao, binafsi sioni tatizo," anasema Henga.

Anasema, wingi wa wanasiasa wa zamani kurudi upya, ni ishara kwamba, wanakubaliana na utendaji wa kiongozi wa sasa wa chama hicho hadi wakaamua kuchukua fomu kutaka uongozi ili wasaidiane naye.

# SIKU 27 KUPIGA KURA KENYA

## Vijana wanavyojiweka kando, huku mitandao ikisheheni taarifa za upotofu, chuki na uzushi

**Na Mwandishi Wetu**



Mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati, ndiye msimamizi mkuu wa kura za uchaguzi wa Rais. **PICHA: MTANDAO**

ZIKIWA zimesalia siku 27 kufikia muda wa kupiga kura, idadi ndogo ya wapigakura na vijana kujiweka pembeni ndiyo mambo yanayoonekana wakati muda unavyosogea na kulikaribia sanduku na karatasi ya kura.

Mwaka jana, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo ya Kenya (IEBC), inayosimamia uchaguzi nchini humo, iliweka lengo la kuandikisha wapiga kura wapya 6,000,000 ili kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu wa mwezi ujao.

Takwimu au data za sensa ya mwaka 2019 zinaonyesha kuwa takriban vijana 5,000,000 wa Kenya walikuwa wamefikia umri wa kupiga kura tangu uchaguzi mkuu wa 2017, hivyo lengo hilo lilionekana kuwa lilikuwa linawakusudia.

Lakini, kampeni ya kuandikisha wapiga kura ilipomalizika Februari mwaka huu, tume ilitangaza kusajili wapiga kura wapya milioni 2.5, vijana wengine zaidi ya milioni 3.5 wako wapi?

Na kwa mujibu wa taarifa zake hivi sasa, kuna wapiga kura milioni nane (8,000,000) waliojiandikisha. Ni karibu theluthi moja ya jumla ya Wakenya milioni 22 walio na umri wa miaka 18 hadi 35 wanaostahili kupigakura. Hali hiyo inadhihirisha kuna kiwango kikubwa kinachoongezeka cha watu wasiojali kuhusu uongozi wa kisiasa na uchaguzi miongoni mwa vijana wapigakura wapya.

### MITANDAO YA KIJAMII

Kenya iko vizuri kwenye matumizi ya mitandao ya kijamii hasa intaneti na imeunganishwa zaidi kuliko mambo yalivyokuwa hapo awali kwenye uchaguzi uliotangulia.

Aidha, ina kiwango cha juu cha watu kuunganishwa na mitandao kama 'Whats App na Facebook, Twitter, Instagram na TikTok' ikiwa na asilimia 87 ya wanaotumia mitandao kwa hivyo idadi ya watu wake inasoma zaidi taarifa za masuala ya kisiasa yaliyoko mtandaoni, lakini changamoto kubwa ni kwamba kuna taarifa potofu na za uchochezi kwenye mitandao ya kijamii ambayo inasomwa na wengi.

Ripoti mpya ya mtafiti Odanga Madung wa Mtandao wa Mozilla inaonyesha kuwa kuna mtandao mmoja matata (jina linahifadhiwa) umejaa kashfa inayotia wasiwasi kuhusu mwenendo mzima wa uchaguzi wa mwaka huu, na jukwaa la mtandao huo linafanya kazi ya kuhabarisha masuala ya kisiasa yanayoonekana haraka na yanayoeneza kwa kasi masuala ya upotoshaji.

Baada ya kuchunguza video kadhaa kutoka akaunti mbalimbali ambazo zilikuwa zimetazamwa kwa wiki moja utafiti ulifichua kuwa hakuna mifumo ya udhibiti wala vitendea kazi (vifaa) vya kukabiliana ipasavyo na taarifa potofu za uchaguzi nchini Kenya zilizoko kwenye mitandao.

Hii imekuwa na athari mbaya kwa wasomaji na watumiaji mitandao hasa vijana, kwani ni wengi wanaotumia jukwaa hilo (jina linahifadhiwa) utafiti unaonyesha kuwa ni vijana wenye umri wa miaka kati ya miaka 14-25.

Jukwaa hilo ndilo programu inayopakuliwa zaidi nchini humo, likipita hata Whats App na Facebook zinazopatikana kila mahali duniani.

Watumiaji mtandao wachanga wanaosoma masuala ya uchaguzi wanazidi kupuuza na kutojihusisha na mchakato rasmi wa kisiasa lakini wakati huo huo , wanakutana na taarifa za kisiasa za uchochezi kwenye jukwaa lao, ikiashiria kuwa kuna matatizo yanayokuja kwenye uchaguzi huo, wataalam wanasema.

"Kwanza, maudhui haya hayako kwenye mtandao mmoja yamesambaa," Madung aliiambia Al Jazeera. "Kwa muda mrefu kabla ya tahadhari kuchukuliwa, taarifa hizo zilikuwa kila mahali kwenye majukwaa makubwa ya mitandao ya kijamii. Shida ni kwamba kuna mtandao ambao unatishia zaidi wakati huu ambao hauna haja ya kuandaa wafuatiliaji ili kueneza habari zake upo kila mahali."

"Sio bahati mbaya ukweli sisi ni wachanga kidemokrasia na kiumri lakini tumeunganishwa zaidi kuliko hapo awali na kwamba tuna idadi kubwa zaidi ya wapigakura ambao hawajaamua kupiga kura lakini hata kujiandikisha. Hali hiyo ni matokeo ya kuimarishwa kwa mazingira ya habari zenye 'silaha' au chuki," anasema Madung

> "Tunagundua kuwa kuna taarifa mitandao ya kijamii na programu zinazofanana zinaendelea kuendesha taarifa za kisiasa ambazo zina silaha ambazo zinaweza kuimarisha au kuongeza watu kutojali wala kuwa tayari kupiga kura. Hasa vijana. Inaongeza hisia kwamba hakuna maana ya kushiriki."

### KUYUMBISHA WAPIGA KURA

Uchaguzi wa mwaka huu una kambi mbili, moja inaongozwa na Waziri Mkuu wa zamani Raila Odinga, ambaye ni kiongozi wa upinzani wa muda mrefu ambaye safari hii anaonekana kama mgombea aliyeidhinishwa na ngazi za juu za mamlaka, au ikulu ikiwa ni pamoja na Rais wa Jamhuri ya Kenya, Uhuru Kenyatta.

Kambi nyingine ni ile ya Naibu Rais William Ruto, ambaye anaonekana kuchukua sauti ya upinzani sasa japo yuko ndani ya serikali, ni kiongozi wa pili kiserikali lakini cha kushangaza anaikashifu muda wote.

Hali hiyo ya kutatanisha, ambayo Rais Kenyatta aliyeko madarakani amevunja uhusiano na Makamu Ruto na kuungana na kiongozi wa upinzani Odinga ambaye alikuwa mkosoaji wake mkali na mpinzani wake mkuu, imewaacha wapiga kura nchini Kenya wakiyumbayumba wasijue lipi la kufanya.

Vijana wengi wapigakura na wazee ambao wameona michezo ya wenyeviti wa vyama vya kisiasa huko nyuma, bado hawajui wafanye nini. Hata katika nchi ambayo mikataba ya kisiasa na ushabiki wa vyama ni jambo la kawaida katika kila mzunguko wa uchaguzi mwaka huu Wakenya wengi wamebaki na maswali bila majibu.

### HOFU KWA TUME

"Taasisi zinazosimamia uchaguzi zinaonekana kutokuwa na maamuzi na huenda kuna kuchanganyikiwa, na kinachojitokeza zaidi ni hisia kwamba matokeo tayari yameshapatikana ni 'mpango uliokamilika ni jambo lililoandaliwa'," anasema mpiga kura mmoja kijana na kuongeza. "Sidhani kama kura yangu itahesabiwa."

Hisia za sehemu kubwa ya wapiga kura ni nini? 'Kila mtu kwenye kugombea uongozi ni fisadi, kwa nini nipige kura? Ni afadhali nisipige kura kuliko kupigia kura uchaguzi na matokeo yako mezani ," Madung anaiambia Al Jazeera.

"Tunagundua kuwa kuna taarifa mitandao ya kijamii na programu zinazofanana zinaendelea kuendesha taarifa za kisiasa ambazo zina silaha ambazo zinaweza kuimarisha au kuongeza watu kutojali wala kuwa tayari kupiga kura. Hasa vijana. Inaongeza hisia kwamba hakuna maana ya kushiriki."

Wataalamu wanasema kuwa taarifa za mitandao zimeingiza sehemu kubwa ya umma kwenye hali ya kukosa hamu wala uwezo au nia ya kujiunga katika kutekeleza majukumu yao ya haki za kiraia ikiwamo kupigakura kuchagua viongozi.

Tuna idadi kubwa ya vijana wenye nguvu ambao kwa kiasi kikubwa hawana hamu wala nia ya kushiriki katika mchakato rasmi wa kisiasa, yaani, kujiandikisha kama mpiga kura na kumchagua kiongozi, " anasema Nerima Wako-Ojiwa, mkurugenzi mtendaji wa Siasa Place, shirika linaloelimisha na kuwawezesha vijana kujihusisha kikamilifu na michakato ya kawaida ya kisiasa kwa kuwapa elimu ya uraia.

"Nina wasiwasi sio tu kwa uchaguzi ujao, lakini kwa mchakato wa demokrasia nchini Kenya kwa upana zaidi, ikiwa vijana wanahisi kuwa wametengwa au haiwahusu kutoka kwenye jukumu au mfumo ambao unapaswa kujumuisha kila mtu si jambo jema," anasema.

"Kwa demokrasia makini kila kura ni muhimu," anaongeza. "Inavyoelekea vijana katika nchi hii hawafikiri hivyo, na nini kinatokea wakati siku moja wataamka na kusema hili ndilo jukumu letu? Sidhani kama tuko tayari kwa ukweli huo."

***AL JAZEERA***

# YALIYOMFIKA BORIS JOHNSON

- Shida si tafrija, tatizo uchumi , maisha magumu
- 'Imekula kwao' baada ya kujiondoa Umoja Ulaya

**Na Ani Jozeni**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza Boris Johnson , hatimaye amebwaga manyanga, baada ya kubanwa na kashfa ya misururu ya tafrija au pati kadhaa katika maskani yake ya 10 Downing Street jijini London, ambayo pia ni ofisi ya Waziri Mkuu, akidaiwa kukiuka miiko ya kudhibiti CORONA .

Ni mtaa wa serikali ambako jumba la kifalme la Buckingham haliko mbali au majengo ya Bunge ya Westminster ambako inaelezwa hekaheka ziliendelea huko kwa siku kadhaa watu wakila na kunywa. Wabunge 39 wenye nyadhifa za uwaziri au unaibu waziri walijiuzulu wakitaka kiongozi huyo aachie ngazi kwa sababu alihusika kwa karibu sana katika kuandaa tafrija hizo.

Kimsingi chama hicho kinaungwa mkono kwa nguvu nchini humo baada ya kufanikisha mkakati wa kuitoa Uingereza katika Umoja wa Ulaya (EU), lakini athari za hatua hiyo pamoja na vita ya Ukraine vimeathiri uchumi wa Uingereza kuliko nchi za Ulaya wanachama wa EU.

**SHIDA SI TAFRIJA**

Baadhi ya wachambuzi wanatoa hisia kuwa hali hiyo ndiyo imemfikisha waziri mkuu huyo mahali pabaya, na siyo mkasa wa kuandaa tafrija hizo, kwani jambo hilo tayari lilikuwa linapita. Hivi majuzi karibu wiki mbili kabla ya kujiuzulu, alipigiwa kura ya kuwa na imani naye kama kiongozi wa kundi la Waconservative au wahafidhina bungeni, chama tawala, akashinda kwa mbinde, halafu ghafla wakamgeuka.

Kwa vile Johnson alikuwa katika mwaka wake wa tatu wa uongozi, na lazima uchaguzi mkuu ufanyike kila baada ya miaka minne kuanzia uchaguzi uliotangulia, bunge linaweza kuvunjwa endapo kuna mabadiliko makubwa, hasa ya uongozi wa chama tawala, ina maana kuna uchaguzi wa bunge mwakani.

Inaelekea kuwa kuharibika kwa hali ya uchumi kwa kiwango kikubwa, chokochoko za migomo ya kutaka nyongeza za mishahara kutokana na kasi ya kupanda kwa bei za vitu, lazima kunaleta wasiwasi wa kuungwa mkono chama hicho cha kihafidhina. Sasa wapigakura na hata wanachama chake cha Conservative wanajua Johnson ni mtu mwenye majibu ya mkato, atawaudhi, tena ana kashfa, hivyo wanahitaji kumuondoa.

Halafu Johnson alikuwa na adhabu inayomngoja katika uongozi wake kwani alimletea taabu Waziri Mkuu aliyemtangulia, Theresa May, wakati akihangaika kupata 'muafaka' wa kujitoa Umoja wa Ulaya unaokubalika kwa washirika wa Ulaya na makundi tofauti ya kisiasa na kitaifa Uingereza.

Johnson alikuwa Meya wa London halafu akawa Waziri wa Mambo ya Nje, akajiuzulu wakati wa majadiliano ya kujiondoa Umoja wa Ulaya Britain Exit (Brexit). Wako waliodhani hata wakati ule kuwa aliongeza mkazo katika misimamo yake dhidi ya kipengele hiki au kile cha makubaliano ya awali aliyokuwa anayafikia May, akilenga kumdhoofisha kisiasa, achaguliwe, aitoe Uingereza EU 'kibabe zaidi.'

Ikabidi mwishowe May ajiuzulu, ukafanyika kwanza mchakato wa kumpata kiongozi mpya wa Conservative bungeni, kwani akishapatikana ndiye anakuwa waziri mkuu. Johnson akashinda mbio hizo na kuingia 10 Downing Street, akavunja Bunge na ukafanyika uchaguzi mkuu mpya yaani wa kuchagua wabunge, chama chake kikashinda kwa kura nyingi, hasa kutokana na yeye mwenyewe kupendwa kwa msimamo mkali kuhusu kujitoa Umoja wa Ulaya.

Hajapata misukosuko mikubwa nje ya suala la COVID-19 ambako aliponea chupuchupu hospitali ya Saint Thomas, na ni sababu mojawapo wengi walishangaa kusikia aliitisha tafrija zinazoweza kueneza UVIKO 19.




Swali linaendelea kukosa jibu tafrija na 'kulakula' pekee ndiko kulimponza Johnson?. **PICHA MTANDAO.**

**NJE NA NDANI KUGUMU**

Kimsingi kuondoka kwa Johnson madarakani ni kile kinachoitwa na wachambuzi wa siasa kuwa ni mkasa wa hulka tu ya kimaisha, kuchukulia vitu muhimu kana kwamba ni mambo rahisi, na hata kutokujali. Ila hakuna ubishi kuwa amekuwa kiongozi mpambanaji mwenye uwezo mkubwa wa kujieleza na kupima mahitaji ya wakati uliopo, lakini mwishowe ikawa ni jambo lisilopingika kuwa wakienda naye kwenye uchaguzi mkuu wataangukia pua, siyo kwa suala tu la kutokujali ila pia kwa hali ya kiuchumi. Na kwa hulka yake, angeendelea kuwatolea nje wapinzani katika masuala ya sera, licha kuwa mara kadhaa 'amesoma ishara za nyakati' akabadili mwenendo, kwa mfano kuacha fadhaa ya ukaribu na wanaoshiriki mapenzi jinsia moja.

Siyo rahisi kusema kama kuanguka kwa Johnson, ambako kumefurahiwa na utawala wa Russia uliosema katika taarifa kuwa ameondoka 'kwa aibu' kwani alikuwa mstari wa mbele kuiunga mkono Ukraine na kupeleka silaha au misaada kwa kadri ilivyoweza kupatikana, kutawezesha mabadiliko halisi Uingereza. Hakuna uelekeo kuwa chama cha Labour kinaweza kupona majeraha ya kuanguka kwa nguvu katika uchaguzi mkuu wa 2019 kwa sababu ya kashfa ya tafrija, na hasa migomo kuhusu misharaha kutokana na kupanda kwa bei.

Tatizo kubwa zaidi liko upande wa utekelezaji wa 'Brexit' ambao sasa unaweka umoja wa Uingereza hatarini, kwani jimbo kuu la kaskazini la Scotland linataka uhuru kwa sauti kali zaidi kuliko awali, ili lifaidi soko huria la Bara la Ulaya. Halafu Ireland ya Kaskazini haitaki masuala magumu kwenye mpaka na Jamhuri ya Ireland Kusini, ambacho ni kipengele cha makubaliano ya amani ya 1998.

Kwa maana hiyo chama cha Conservative cha Johnson , kinajua kina kazi ngumu mbele yao kulinda mkataba au muafaka na Ulaya halafu walinde pia mikataba yao ya ndani ya umoja wa jina kubwa la 'Great Britain' ambayo malkia anaelekea ukingoni, na mwanae, Prince Charles hana nafasi katika mioyo ya watu kama alivyo Malkia Elizabeth II.

Imefikia mahali hata Australia, Canada na New Zealand wanafikiria kuingia mfumo wa Jamhuri na hakuna uhakika nini kitafuata endapo Malkia Elizabeth akiondoka wakati wowote itakuwaje na Chama cha Conservative kinataka angalau kuwe na mtu mwingine ambaye akiongea watu watamsikiliza.

Ndiyo kimsingi siyo tatizo la hizo tafrija, ni uchumi kuyumba kwa upande mmoja, na kutetereka kwa misingi ya umoja wa nchi kwa upande huo.

> "Inaelekea kuwa kuharibika kwa hali ya uchumi kwa kiwango kikubwa, chokochoko za migomo ya kutaka nyongeza za mishahara kutokana na kasi ya kupanda kwa bei za vitu, lazima kunaleta wasiwasi wa kuungwa mkono chama hicho cha kihafidhina. Sasa wapigakura na hata wanachama chake cha Conservative wanajua Johnson ni mtu mwenye majibu ya mkato, atawaudhi, tena ana kashfa, hivyo wanahitaji kumuondoa.





## Vijana wapewa mbinu kujiajiri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kuwa wabunifu kutokana na taaluma wanazosomea katika vyuo vya elimu ya ufundi nchini ili kubaini soko la ajira.

Mkuu wa Chuo cha Don Bosco jijini Dodoma, Dk. Justine Mulebya, alisema hayo jana kwenye kongamano la 'Career Fair' la mwaka 2022 lililofanyika katika viwanja vya chuo hicho kwa kushirikisha wadau na wanafunzi wanaosoma fani mbalimbali.

Dk. Mulebya alisema vijana wakiweka jitihada kwenye ubunifu na ujuzi itawasaidia kujiajiri wao wenyewe badala ya kusubiri ajira kutoka serikalini au sekta binafsi.

"Vijana mnatakiwa kuwa wabunifu na wenye weledi mkifanya hivyo, itawasaidia kujikwamua kiuchumi kutokana na kwamba mtakuwa mmebaini soko la ajira, lakini pia kuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe," alisema.

"Nasisitiza wanafunzi kuwa wabunifu zaidi pale wanapokuwa darasani kwenye masomo yao, tunahitaji kuona vijana wanachangamkia soko la ajira mara wanapohitimu masomo yao," alisisitiza.

Mkuu huyo alisema vyuo vya ufundi vinasaidia katika utoaji taaluma za ufundi, hivyo wanafunzi wanapaswa kuzingatia kile wanachofundishwa na kuongeza ubunifu zaidi.

Naye Meneja wa Hoteli ya Dodoma, Wilington Maleya, aliwataka wanafunzi kuweka jitahada katika masomo ya nadharia na vitendo ili kuendana na soko la ajira.

Alishauri chuo hicho kiwe na kitengo cha kuwafuatilia wanafunzi wao ili wajue huko walipo wanafanya nini, baada ya kuhitimu masomo yao.

Mkurugenzi wa Chuo hicho, Father Boniface Mchami, alisema chuo hicho kimekuwa kinatoa kozi mbalimbali za ufundi ikiwamo ufungaji umeme, nishati ya jua na umeme, kuchomelea, ufundi magari, mwashi, ufundi bomba, chakula na vinywaji, utayarishaji wa vyakula na kilimo ubunifu na teknolojia.

Mratibu wa mafunzo na malezi wa vijana katika chuo hicho, Anansia Lema, alisema kuwa lengo la kongamano hilo ni kuwaunganisha vijana na wadau walio kwenye soko la ajira ili kubadilishana mawazo.

# Mpango kukomesha mauaji waiva

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KUTOKANA na kukithiri kwa mauaji ya wenza nchini, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinatarajia kutoa ripoti yake Novembe 29, mwaka huu, itakayosaidia kushirikiana na serikali kutoa elimu kwa umma ili kuondokana na tatizo hilo.

Ripoti yake ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora kwa mwaka 2019 na 2020, inaonyesha wanawake 44 waliouawa na wapenzi wao wa karibu huku wivu ukiwa chanzo kikuu cha mauaji hayo.

Julai, mwaka jana, Jeshi la Polisi Tanzania liliripoti kuwa katika kipindi cha miezi miwili lilikamata watu 275 wanaohusishwa na mauaji, yakiwamo matukio 21 ya wenzi yaliyochochewa na wivu.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Wakili Anna Henga, aliyasema hayo jana baada ya kikao cha ujumbe wa kituo hicho na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, jijini hapa.

Alisema ripoti za kituo hicho kwa mwaka 2020 na 2021 zinaonyesha mauaji ya wenza yamekuwa yakiongezeka, kutokana na hali hiyo imewasukuma kuanza kukusanya taarifa na takwimu ili kuandaa ripoti maalum kuhusu suala hilo.

"Tumeongea masuala mazima ya ukatili wa kijinsia, ustawi wa jamii, kuelimisha umma kuhusu masuala ya mauaji ya wenza ambayo yamekithiri sana Tanzania, tufanye kazi kwa pamoja kwa ajili ya kutetea haya makundi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu ili yaweze kupata haki zao," alisema.

Alibainisha kuwa wamekubaliana kutokana na mwongozo mzuri ambao utafanyiwa kazi na asasi zingine za kiraia.

"Tunataka kuanza kuandaa huu mwongozo, study ya mauaji ya wenza itazinduliwa Novemba 29, mwaka huu, lakini huu mwongozo itakuwa kabla study," alisema.

Akizungumzia kikao na Waziri Gwajima, alisema wamekutana kujadili masuala mbalimbali ya maboresho kuhusu haki za makundi hayo.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuhuwisha mahusiano na wizara hiyo kwa sababu wana mkataba wa kuendelea kutetea makundi hayo na wamezungumzia Mpango wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na ustawi wa jamii.

Kwa upande wake, Waziri Gwajima alisema uwapo wa madawati mengi ya kijinsia nchini umesaidia kusikika kwa matukio ya ukatili.

Dk. Gwajima alisema kuendelea kusikika kwa matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hapa nchini inatokana na serikali kufungua madawati mengi ya kijinsia maeneo mbalimbali.

"Kumekuwa na kuongezeka kwa kuripotiwa kwa matukio ya ukatili wa kijinsia tunaweweza kusema kuwa hayo ni sehemu ya mafanikio kwa sababu serikali ilikuwa na mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto," alisema.

Alisema mwaka 2021 matukio 11,499 ya ukatili kwa watoto yaliripotiwa ni tofauti na miaka ya nyuma ambapo matukio yalikuwa yakifanyika hayaripotiwi.

Waziri huyo alisema walitarajia mpaka mwaka 2022 kuwa na kamati kwenye jamii 20,750 lakini kati ya hizo zimeundwa kamati 18,186 sawa na asilimia 88.

Pia alisema madawati ya kijinsia kwenye vituo vya polisi yameimarishwa.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akizungumza na ujumbe wa Kituo cha Haki za Binadamu uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga (kushoto), walipofika ofisini za wizara hiyo, Mtumba jijini Dodoma jana, kujadiliana masuala ya kiutendaji. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainabu Chaula. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# BAKWATA kuzindua mfuko kuwasaidia wajane na yatima

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma linatarajia kuzindua mfuko kwa ajili ya kuwasaidia wajane na yatima ili kujiunga kwenye vikundi vitakavyowasaidia kujishughulisha na ujasiriamali.

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema hayo alipokuwa akizungumza na wajane na yatima katika ibada maalum iliyoambatana na kuliombea taifa kwenye msikiti wa Gaddafi, jijini hapo.

Alisema fedha kiasi cha Sh. milioni 10 walizopokea kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan zitatumika kuwawezesha wajane na yatima hao kupitia vikundi vya ujasiriamali.

"Napenda niwaambie bibi zangu na mama zangu kuwa hivi karibuni tunatarajia kuzindua mfuko kwa ajili ya wajane na yatima ili muweze kuungana kwa pamoja na muanzishe ujasiriamali kupitia fedha hizo.

"Tunatakiwa sisi zote kama tulivyo hapa ndani ya uislamu wetu kumshukuru na kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha hizo Sh. milioni 10 kwa ajili yenu," alisema.

Alisema kupatikana kwa fedha hizo ni matumaini yao wajane na yatima wataachana na kutegemea kuombaomba.

Pamoja na hayo, aliwataka wajane na yatima hao wa dini ya kiislamu kuhakikisha wanashiriki katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema kuwa suala la kushiriki katika sensa ya watu na makazi kwa upande wao ni muhimu kwa Watanzania wote wakiwamo wajane na yatima ili kuwasaidia viongozi na serikali jinsi ya kupanga bajeti yake.

"Suala la kuhesabiwa ni muhimu maana linafanya wepesi kwa viongozi kujua wanaweza kutoa huduma kwa watu wangapi na uwiano gani ikiwa ni pamoja na kutambua mahitaji ya makundi maalum," alisema.

Mwenyekiti wa Wajane Mkoa wa Dodoma, Rahma Mohammed, alisema wajane kama watashikamana wakatumia fursa wanazopata kupitia uongozi wa msikiti wa Gaddafi watajikwamua kiuchumi.





# Operesheni kabambe ukaguzi wa malori yaanza nchi nzima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, limeanzisha operesheni maalumu ya kukagua malori ya mizigo nchi nzima ili kukabiliana na ajali ambazo zimekuwa zikisababishwa na magari hayo.

Operesheni hiyo imeanzia katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ikiongozwa na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa.

Operesheni hiyo ilianza juzi mkoani Mbeya na Kamanda Mutafungwa alisema lengo ni kudhibiti ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu na kuharibu mali.

Alisema katika operesheni hiyo mkoani hapa, walikagua malori 195 kwa ushirikiano na wakaguzi kutoka ofisi za wakuu wa usalama barabarani mikoa ya Mbeya, Songwe na Njombe.

Kati ya malori hayo yaliyokaguliwa, alisema 53 yalibainika kuwa ni mabovu, hivyo yalizuiwa kuendelea na safari mpaka yatakapokuwa yametengenezwa na kukaguliwa tena.

Alisema malori hayo yalibainika kuwa mabovu kwenye mifumo ya breki na usukani hali ambayo alisema inahatarisha maisha ya madereva, watumiaji wengine wa barabara pamoja na mali zinazokuwa zinasafirishwa kwenye magari hayo.

"Lori la mizigo likiwa bovu kwenye mifumo ya breki na linapita kwenye mikoa hii ambayo ni ya milima na miteremko mikali ni hatari sana. Kwa hiyo haya hayaruhusiwi kuondoka mpaka yatengenezwe," alisema Mutafungwa.

Aliagiza wamiliki wote wa malori kuhakikisha wanayakagua kabla hawajayaruhusu kwenda kubeba mizigo huku akiwataka madereva pia kuhakikisha mifumo ya magari wanayoendesha inakuwa imara.

Alisema operesheni hiyo ya ukaguzi wa malori itakuwa endelevu kwa nchi nzima na kwamba baada ya kukamilisha watafanya tathmini na kutoa taarifa ya hali halisi ya malori hayo.

Baadhi ya madereva walisema wamekuwa wakilazimika kuendesha magari hayo kutokana na wamiliki kuwalazimisha kuendesha hata kama ni mabovu, hivyo wakalishukuru Jeshi la Polisi kwa kuanzisha operesheni hiyo.

Mmoja wa madereva hao, Seleman Majuto, alisema mara nyingi madereva wamekuwa wakilaumiwa linapotokea tatizo barabarani lakini chanzo kikubwa ni wamiliki ambao huwa hawataki kuyafanyia matengenezo magari yao.

Alisema ukaguzi huo unaofanywa na Jeshi la Polisi, utawasaidia kuwakumbusha wamiliki wa malori ambao wamekuwa wakigoma kutengeneza magari.

Naye George Sanga alisema yeye ni miongoni mwa waliozuiwa kuendelea na safari kutokana na gari lake kuwa bovu na kwamba gari analoendesha magurudumu yameisha.

Alisema wakati mwingine matajiri huwa wanawatishia kwamba wasipoendesha magari hayo kwa kisingizio cha ubovu wa mifumo wanawafukuza kazi na kuajiri wengine.

# Vijana wa CHADEMA waonywa kuhusu matusi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, umewataka wanachama wa chama hicho kuvumiliana kwenye mitandao ya kijamii kwa kuacha kutukanana.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa Mkutano maalumu wa chama Wilaya ya Mbeya Vijijini ambapo alisema baadhi ya vijana wamekuwa wakitukana mitandaoni.

Alisema chama hicho kimekuwa kikijipambanua kwa wananchi kuwa ndicho kitakuwa mbadala wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) lakini matusi ambayo yaandikwa na vijana hao yamekuwa yakionyesha utovu wa nidhamu.

Alisema kwa muda mrefu chama hicho kimekuwa kikipigania haki za Watanzania lakini kitendo cha kuanza kutukanana mitandaoni kinaharibu nia njema ya chama hicho.

"Tunaposema sisi ni bora kuliko CCM ni lazima tuonyeshe kuwa ni wasafi, sasa kuna baadhi ya vijana wanatukana matusi mitandaoni na wakati mwingine wanawatukana hata viongozi, hiyo tabia naomba iishe," alisema Msigwa.

Alisema chama hicho kina wasemaji wakuu lakini baadhi ya wanachama wamekuwa wakisema kama vile wao ndio wasemaji wa chama na hivyo akawataka kuacha tabia hiyo.

Alisema viongozi wa chama hicho wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kukijenga chama wakitumia raslimali zao binafsi lakini baadhi ya wanachama waliokuwa na uvumilivu wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kuharibu chama.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alipiga marufuku vijana wa chama hicho kutukana mitandaoni huku akiwataka kukosoana kwa staha.



Mkuu wa Mauzo wa Kampuni ya Mikopo ya Platinum Credit Tanzania, Grace Crispin, akikabidhi taulo za kike kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kujisitiri wakati wa hedhi, taulo hizo zilikabidhiwa juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walanguzi wa tumbaku wavamia Chunya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU) kimelalamikia uwapo wa walanguzi wa tumbaku wanaodai wametumwa na viongozi wa juu kwenda kununua zao hilo kutoka kwa wakulima binafsi bila kupitia kwenye vyama vya msingi.

Akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Dharura ulioitishwa kwa lengo la kujadili suala hilo, Mwenyekiti wa CHUTCU, Sebastian Masika, alisema katika msimu huu wa ununuzi wa tumbaku, wameibuka watu wanaokusanya tumbaku kutoka kwa wakulima wanaojiita binafsi jambo ambalo ni kinyume cha utaratibu.

Masika alisema watu hao wanaonunua tumbaku kutoka kwa watu wanaojiita wakulima binafsi, wanadai wametumwa na kampuni iitwayo Amy Holdings Company ambayo hivi karibuni ilitambulishwa na uongozi wa mkoa wa kuwa itaanza kununua tumbaku ya wakulima kuanzia msimu ujao.

Masika alisema kuwa kilimo cha tumbaku ni cha mkataba ambapo wakulima kupitia vyama vya msingi wanakopeshwa mbolea na pembejeo nyingine kutoka kwenye taasisi za kifedha na kisha wanalipa mikopo yao kwa kukatwa fedha baada ya kuuza mazao yao kwenye vyama vya msingi.

Alisema kitendo cha kuibuka walanguzi hao kitasababisha wakulima kutorosha tumbaku na kuiuza bila kupitia kwenye vyama vya msingi jambo ambalo litapelekea madeni ya pembejeo kutolipika.

"Madeni haya yasipolipika, benki zinazotukopesha zinashindwa kurejesha fedha zao, hivyo zitakosa imani ya kuendelea kukopesha wakulima katika msimu unaofuata. Madhara yake ni kwamba vyama vya msingi vitakufa, wakulima hawatakopeshwa tena, hivyo uzalishaji wa tumbaku msimu ujao utashuka," alisema.

Masika aliiomba serikali kuingilia kati kwa kuwakamata wahusika na kuzuia ununuzi wa tumbaku nje ya utaratibu ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.

Baadhi ya wajumbe wa mkutano huo, walishangazwa na kuibuka kwa watu wanaonunua tumbaku bila kupitia kwenye vyama vya ushirika wakidai kuwa tayari serikali ilishapiga marufuku tabia hiyo.

"Nikirejea kwenye kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa soko la tumbaku la msimu huu katika Kijiji cha Bitimanyanga, aliagiza walanguzi na watoroshaji wa tumbaku wakamatwe na kuchukuliwa hatua, sasa nashangaa hawa wanaolangua tumbaku hadharani mbona hawakamatwi?" Alihoji Mwenyekiti wa Lupa AMCOS, Masingija Jilala.

Alisema ghala linalotumika kuhifadhi tumbaku inayonunuliwa kwa ulanguzi bila kupitia chama cha msingi liko kwenye kijiji chake na alishaamua kwenda kwenye ghala hilo kuzuia, lakini alipofika alielezwa kuwa wanaonunua tumbaku hiyo wanapata maagizo kutoka ngazi za juu.

"Pengine hata mimi nashawishika kuamini kuwa wanaofanya vitendo hivi wameagizwa kutoka kwa viongozi wa juu maana licha ya Mkuu wa Mkoa kukataza, watu hawa wanalangua tumbaku hadharani, polisi wanashindwa kuwakamata licha ya kwamba nisharipoti suala hili kituoni," alisema Jilala.

Mwakilishi wa Bodi ya Tumbaku Mkoa wa Mbeya, Resujak Kimiri, hawana taarifa za uwapo wa mnunuzi mpya wa tumbaku msimu katika Mkoa wa Kitumbaku wa Chunya.

Alisema bodi imefuatilia makao makuu na kuthibitishiwa kuwa hakuna mnunuzi mpya aliyepewa leseni ya ununuzi wa tumbaku msimu huu katika Mkoa wa Kitumbaku wa Chunya zaidi ya Kampuni ya Premium ambayo ndiyo yenye haki ya kununua tumbaku hiyo.

"Niwathibitishie kama kuna kampuni nyingine zaidi ya Premium ambayo inanunua tumbaku hapa Chunya ni walanguzi maana hakuna leseni nyingine ya ununuzi wa tumbaku iliyotolewa hapa, hivyo hao ni wahalifu kama wahalifu wengine," alisema Kimiri.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alikiri kuwa serikali imemtafuta mnunuzi mwingine wa tumbaku wilayani Chunya kwa nia ya kuongeza ushindani wa bei kwa wakulima.

Hata hivyo, alisema kuwa mnunuzi mpya aliyepatikana anapaswa kuanza kununua tumbaku kuanzia msimu ujao, ingawa kama kutakuwapo na tumbaklu ya ziada ambayo mnunuzi aliyepo atashindwa kuinunua basi kampuni hiyo itaruhusiwa kuinunua.

"Nawaomba wananchi waelewe kuwa serikali inayo nia njema ya kuhakikisha wakulima wananufaika kwa kuuza tumbaku yao kwa bei nzuri yenye ushindani. Hata hivyo tutasimamia kuhakikisha wanunuzi wote wanafuata taratibu za ununuzi wa zao hilo," alisema Mayeka.

# Rais Samia kufungua kongamano la Mkapa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufungua kongamano la kumbukizi ya miaka miwili ya mwasisi wa Taasisi ya Mkapa Foundation, Hayati Benjamin Wiliam Mkapa, litakalofanyika mjini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benjamin Mkapa Foundation (BMF), Dk. Ellen Senkoro, alisema kongamano hilo litahudhuriwa na viongozi wa ngazi mbalimbali kutoka Tanzania na nje ya Tanzania. Kaulimbiu ya kongamano hilo ni 'Urithi Kutoka kwa Mkapa, Uongozi Shupavu katika Kuchochea Mabadiliko kwa Wote'.

Dk. Senkoro alisema kongamano hilo la siku mbili litaanza leo na kesho litahitimishwa na kufungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. Mada mbalimbali zitawasilishwa ikiwamo jinsi ya kuongeza kasi katika mikakati mabadiliko ya sekta ya afya Tanzania kupitia ushirikia wa biashara na sekta binafsi.

Alisema pia mjadala wa kongamano hilo utaongozwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Maoud Othman.

Mada ya pili itakayowasilishwa ni ubunifu katika mikakati na ushirikiano kati ya taasisi za serikali na za binafsi katika kufikia malengo ya kutoa huduma ya afya kwa wote.

"Tunapenda kutoa shukurani za dhati kwa serikali zote mbili pamoja na wadau wote ambao wameendelea kushirikiana nasi katika kufanikisha kongamano hilo, tunapenda kutambua mchango wa hali na mali kutoka kwa wafadhili ikiwamo IPP Media," alisema.

Pia alisema tokea kuanzishwa kwa taasisi hiyo ni miaka 16 na lengo lake lilikuwa kuimarisha huduma za afya hasa mapambano dhidi ya UKIMWI lakini kwa sasa wamejikita katika huduma zote za afya ikiwamo huduma ya mama na mtoto na mapambano ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema taasisi hiyo imeajiri watumishi 4,100 na kuwasambaza katika vituo vya afya na hospitali mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wananchi na kuchangia kupunguza tatizo la upungufu wa wataalamu wa afya.

Taasisi hiyo, alisema imeimarisha miundombinu ya taasisi ya afya ikiwamo kujenga nyumba 482 za wataalamu wa afya 482 katika wilaya 52 Tanzania Bara ili kuboresha huduma za afya ya jamii na kuwafanya watumishi wa afya kuishi vijijini karibu na jamii.

# Mwinyi aipa heko Benki ya Dunia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya Dunia kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Rais Mwinyi alitoa pongezi hizo jana Ikulu Zanzibar, alipofanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa.

Makamu huyo wa rais alifika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha sambamba na kueleza jinsi ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya benki hiyo.

Katika pongezi hizo, Rais Mwinyi alisema Benki ya Dunia ina historia ya muda mrefu katika kuiunga mkono Zanzibar katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizoathirika na UVIKO -19 hasa kupitia sekta ya utalii ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa.

Hata hivyo, alisema kwamba hivi sasa shughuli za utalii nchini zimekuwa zikiimarika kila uchao kutokana na kutokuwapo kwa janga la UVIKO-19 hatua ambayo inasababisha watalii kutoka nchi kadhaa duniani kuitembelea Zanzibar.

Pia Rais Dk. Mwinyi alimweleza kiongozi huyo hatua zilizofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza miradi ya elimu na afya inayotokana na fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kushughulikia huduma za jamii.

Rais Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuishukuru na kuipongeza Benki ya Dunia kwa kuendelea kuisaidia Zanzibar katika miradi yake ya maendeleo huku akieleza vipaumbele vilivyowekwa na serikali yake hivi sasa katika kuimarisha miundombinu ikiwamo barabara na bandari pamoja na kuimarisha sekta ya uchumi wa buluu.

Alieleza jinsi uchumi wa buluu ulivyochukua nafasi kubwa katika sekta ya utalii, uvuvi, kuwasaidia kinamama wanaojishughulisha na kilimo cha mwani, bandari pamoja na sekta nyinginezo.

Rais Dk. Mwinyi alieleza hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuhakikisha zao la mwani linapata thamani na wakulima wake wanafaidika na kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kujenga kiwanda cha kusarifu mwani Chamanangwe, kisiwani Pemba.

Alisema serikali anayoiongoza imeweka kipaumbele na kutilia mkazo uimarishaji wa elimu, maji, miundombinu ya barabara na huduma za kijamii na kwamba juhudi zinazochukuliwa katika suala zima la kuongeza nishati ya umeme Zanzibar.

Naye Kwakwa alimweleza Rais Dk. Mwinyi jinsi Benki ya Dunia inavyofarijika na juhudi za serikali ya Zanzibar katika kuendeleza na kuimarisha miradi ya maendeleo inayosimamiwa na benki hiyo.

Alisema hatua zinazochukuliwa na benki hiyo katika kuhakikisha Zanzibar inafaidika kwa mara nyingine tena na fedha za utekelezaji miradi ya maendeleo kupitia dirisha jipya la Jumuiya ya Kimataifa ya Maendeleo (IDA 20).

Katika mazungumzo hayo, Kwakwa alimhakikishia Rais Dk. Mwinyi kwamba Benki ya Dunia itaendelea kuunga mkono miradi ya maendeleo iliyopewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwamo miundombinu ya barabara pamoja na sekta nyinginezo.

Alisema Benki ya Dunia imekuwa na ushirikiano mkubwa na Zanzibar katika nyanja mbalimbali za kijamii na kiuchumi ikiwamo ujenzi wa miundombinu, elimu, afya, mazingira na mengineyo mingi kupitia mpango wa mikopo nafuu.

Pia alimweleza Rais Dk. Mwinyi kwamba janga la UVIKO-19 limeathiri kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi kwa nchi kadhaa zinazotegemea sekta ya utalii na kueleza matarajio yake kwamba Zanzibar itarudi katika hali yake ya mwanzo.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid (kushoto), akizungumza na Waziri wa Uchumi wa Buluu, Suleiman Makame, katika kijiji cha Muungoni Mkoa wa Kusini Unguja wakati uongozi wa Benki ya Dunia ulipofika kukagua miradi ikiwamo ya ukulima wa mwani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ukaguzi wabaini ubovu majengo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhammed Said, amesema ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe mwaka 2019/20, imebainika kuwa majengo 127 ya mji huo yako katika hali mbaya.

Amesema kati ya hayo, majengo 36 yako katika hali mbaya zaidi yakiwamo yanayomilikiwa na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Fedha na Mipango, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, watu binafsi na Shirika la Nyumba la Zanzibar.

Aliyasema hayo jana akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Kikwajuni mjini Zanzibar wakati akitoa taarifa kuhusu uwekezaji katika Mji Mkongwe wa Zanzibar.

"Mtakumbuka kuwa Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi baada ya kuingia madarakani alikutana na wadau wa Mji Mkongwe waliojumuisha wakazi, wafanyabiashara, wapenzi, watumiaji na wataalamu. Moja kati ya maoni yaliyotolewa ni kufunguliwa fursa ya uwekezaji katika eneo la Mji Mkongwe," alisema.

Waziri Simai alisema maoni hayo yametokana na hali mbaya ya majengo na mazingira yake na hasa ikizingatiwa kuwa na wamiliki wakazi hawana uwezo wa kuyakarabati kwa sababu ya gharama kubwa jambo linalosababisha kupungua kwa hadhi ya mji pamoja na kusababisha maafa kwa watumiaji.

Alisema kutokana na maoni yaliyotolewa, serikali iliamua kutoa fursa ya uwekezaji kwa lengo la kuimarisha hali na hadhi ya majengo na maeneo ya Mji Mkongwe kama ilivyoshauriwa na wananchi.

"Katika utekelezaji wa mpango huo, kwa kushirikiana na wamiliki wa majengo, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilitoa matangazo kupitia vyombo vya habari pamoja na tovuti ya wizara na tovuti ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa ajili ya kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kwa kufuata taratibu zilizopo za uwekezaji," alisema.

Alisema wizara imepanga kutoa fursa ya uwekezaji kwa awamu kwa ajili ya kupatikana ufanisi mzuri wa utekelezaji wa uwekezaji ndani ya Mji Mkongwe na kuunda kamati maalumu inayoshughulikia uwekezaji ndani ya Mji Mkongwe.

Kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, alisema mwekezaji analazimika kujaza fomu ya uwekezaji na kulipa fedha za utangulizi ndani ya mwezi mmoja baada ya kukubaliwa maombi yake na ambao hawatakamilisha taratibu, wizara hufanya mawasiliano nao na ikishindikana huyatangaza upya majengo hayo kwenye awamu nyengine.

Pia alisema mwekezaji baada ya kukamilisha utaratibu wa malipo ya fedha za utangulizi anatakiwa kuwasilisha ramani za asili na za mapendekezo (existing and proposed drawing) kwa ajili ya kupasishwa na mamlaka na baada ya hapo hupewa vibali vya ujenzi.

Alieleza kuwa vibali vya ujenzi vinatolewa baada ya kuhakikisha kuwa michoro husika inaendana na miongozo ya uhifadhi kwa vile mji huo upo kwenye orodha ya urithi duniani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 76 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late JAPHET DANIEL MASOLWA**

**By 1. DANIEL JAMES MASOLWA**
**2. ........................................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **18th day of July..... 2022**

Dated at MOROGORO this **01 day of July...2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA KWA VYETI



**HABIBA RAMADHANI SULUTA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **No. S0203-0077** kilichotolewa na baraza la mtihani kupitai **IRINGA GIRLS' SEC. SHOOL** Mwaka 2009, Cheti cha chuo No. **Ns0203/0077/2009** kilichotolewa na **CHUO CHA UALIMU BUSTANI** mwaka 2018. Yeyote atakaeviona atoe taaria kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/274473/2022. DOD/DOD/RB/274474/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMANUEL LUKAS KOMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KUZALIWA/HATI YA KUSAFIRIA/CHETI CHA KIDATO CHA NNE INDEX **NO.S1220-0122** (MSAMALA-2009) / CHETI CHA KIDATO CHA SITA INDEX **NO.S0338-0583** (NDANDA-2012) CHETI CHA BACHELOR IN SOCIOLOGY **REG.2012/0970** (JORDAN-2015) TRANSCRIPT BACHELOR IN SOCIOLOGY/CHETI CHA MASTER'S IN SOCIOLOGY **REG.2016/0078** ,TRANSCRIPT MASTER'S IN SOCIOLOGY VIMEPOTEA KWA PAMOJA. YEYOTE ATAKAE VIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI AU **PIGA SIMU NAMBA 0677731328. DSM/PHQ/RB/243113/2022.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamiziwa mirathi Na 37/2022**

**MWAJABU SEKALINGA............................Marehemu**
**KENNANY MBEYELA.................................Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa watu wote wanaodai kuwa na haki na marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 11 ya mwezi agosti mwaka 2022.

Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 11 Julai mwaka 2022.

Hakimu Mkazi

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU PETER BUJIJI MADELELE**anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T753AGT** aina ya **TOYOTA COROLLA,** Rangi Nyeupe. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/238542/2022**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**MWANAHAMISI ISSA MLALIKWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA NYUMBA **(RIVERSIDE, MWEMBESONGO)** SQUATER 18, YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI AU PIGA SIMU NAMBA **0782408992 DSM/PHQ/RB/207297/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**Elina paul sankele** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1559-0027** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **BAOBAB SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti cha kidato cha sita chenye ndex namba **S0264-0082** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **BARBRO JOHANSSON GIRLS SCHOOL** mwaka 2020. Yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **KBD/RB/1072/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEWICE RESTIDIUS CHENKUNGU,** Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha Kidato cha Nne Chenye Index no **S.2237/0030** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Shule ya Kihanga Secondary School Mwaka **2018**, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Taarifa ya Polisi:**
**RB NODOD/DOD/RB/250657/2022**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **CITI BANK TANZANIA , Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara Jenereta **(GENERATOR)** iliyoko kwenye jeduali, mnada utafanyika Tarehe **20/07/2022,** katika yard yetu iliyopo Tabata Kimanga kuanzia saa mbili asubuhi,

| SERIAL NO. | MODEL | CAPACITY |
|---|---|---|
| GD03-4559040 | CUMMINS-F10KBGS990 | KVA 550 |

**MASHART YA MNADA**
Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi,Genereta linauzwa kama liilivyo,Ukaguzi utaanza Tarehe **15/07/2022**

**MAWASILIANO PIGA: -**
**0715-683777/0782548337**
**info@sepcoauctioneering.co.tz**
**www.sepcoauctioneering.co.tz**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMZA SULEIMAN ISSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T509 BKD** chasisi namba idapaj**11290011141**, engine namba **156fmid5090731,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/276343/2022**

**EXTRACT FROM BOARD MEETING OF LEMAMO LIMITED OF P.O.BOX 1016 DAR ES SALAAM HELD ON THE 8TH DAY OF JULY 2022**

**BOARD RESOLUTION**

At the Board of Director's meeting of **LEMAMO LIMITED** held at the registered office, on the 8th day of July 2022, the Board members of the company, with registration number 110001, having assessed the status of the company, have hereby duly passed a Special Resolution to do the following:

1) To wind up the Company voluntarity in accordance with Section 333(1) of the Companies Act No. 12 of 2022;
2) The Company confirms that there are no reasons to prevent the dissolution of the company; and,
3) The Company has appointed **NOEL BERNARD SABUNI** of **LYNO ASSOCIATE**, as the liquidator for the purpose of winding up of the Company.

Certified true copy

.........................................
Elibariki Robert Magembe
Director
8th July 2022

.........................................
Catherine Sia Magembe
Director
8th July 2022

LEMAMO LIMITED
P. O. BOX 1016
DAR ES SALAAM
TANZANIA

.........................................
Beatrice Alice Magembe
Director
8th July 2022

.........................................
Mary Rose Mgema
Company Secretary
8th July 2022


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais wa Sri Lanka atafuta njia kutoroka

**COLOMBO,** SRI LANKA

RAIS wa Sri Lanka, Gotabaya Rajapaksa inaelezwa kuwa anatafakari kulikimbia taifa hilo la kisiwa kwa kutumia boti ya doria ya jeshi la wanamaji.

Hatua ya kutoroka inatokana na kuwepo kwa tofauti kati yake na maofisa wa uhamiaji katika uwanja wa ndege. Rajapaksa ameahidi kujiuzulu leo na kupisha njia ya kukabidhi madaraka kwa amani kufuatia maandamano makubwa dhidi yake kupinga mdororo wa uchumi nchini humo.

Maofisa walisema rais huyo mwenye umri wa miaka 73 alitaka kusafiri kwenda Dubai.

Akiwa rais, Rajapaksa ana kinga ya kukamatwa, na inaaminika anataka kwenda ng'ambo kabla ya kujiuzulu ili kuepusha uwezekano wa kukamatwa.

Hata hivyo, maofisa wa uhamiaji walikataa kwenda katika eneo la wageni mashuhuri kupiga muhuri kwenye paspoti yake, wakati akisisitiza kuwa hawezi kutumia maeneo ya wasafiri wa kawaida akihofia kushambuliwa.

Kaka yake mdogo, Basil Rajapaksa aliyejiuzulu kama waziri wa fedha mwezi Aprili, aliikosa ndege yake mapema jana kwenda Dubai baada ya kuwepo kwa vikwazo katika uwanja wa ndege. **BBC**

# Uchunguzi waonyesha Dos Santos hakuuawa

**LUANDA,** ANGOLA

MWANASHERIA Mkuu wa Angola, Helder Pitta Gros, amesema uchunguzi wa maiti ya aliyekuwa Rais wa Angola Jose Eduardo dos Santos, umedhibitisha hakuuawa kwa sumu.

Mahakama ya Barcelona nchini Hispania iliidhinisha kufanyika kwa uchunguzi wa maiti kufuatia ombi la binti wa Santos, Tchize dos Santos, ambaye alidai kuwa baba yake aliuawa.

Dos Santos alifariki katika hospitali ya Barcelona siku ya Ijumaa, ambako alikuwa akipatiwa matibabu.

Mawakili wa familia hiyo walishutumu hatua za serikali ya Angola kurudisha mwili wa marehemu nyumbani kwa ajili ya mazishi ya kiserikali, wakisema walitaka mazishi ya kibinafsi nchini Uhispania. **BBC**

# Ukraine yaanza kujibu mashambulizi ya Russia

**KYIV,** UKRAINE

JESHI la Ukraine limesema limeanza operesheni ya kujibu mashambulizi dhidi ya vikosi vya Russia wanaodhibiti sehemu ya eneo la kusini la Kherson.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alithibitisha hayo wakati akitangaza kuuliwa kwa raia wa Ukraine katika shambulizi la roketi lililofanywa na Russia.

Kamandi ya kusini ya jeshi la Ukraine imesema ghala la silaha la Russia lililengwa katika mji wa Nova Kakhovka, ambako kuna mtambo wa kufyatulia makombora na vifaa vya jeshi ambavyo viliharibiwa na kuwapoteza wanajeshi wake zaidi ya 50, kwa mujibu wa Ukraine.

Ghala hilo liko kilomita 55 mashariki mwa mji muhimu wa bandari wa Kherson katika Bahari Nyeusi, ambalo linadhibitiwa na vikosi vya Russia. Video katika mtandao wa kijamii umeonyesha mlipuko mkubwa.

Shirika la habari la Russia (RIA) Novosti mapema asubuhi limeripoti kwamba watu wapatao saba wameuliwa, wanne hawajulikani waliko na wengine kadhaa wamejeruhiwa kufuatia shambulizi hilo.

Zelensky athibitisha vifo vimeongezeka

Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la RIA Novosti watu wengi walizikwa kwenye vifusi na mamia ya makazi yakaharibiwa. Haikuwezekana mara moja kuthibitisha kauli zilizotolewa na pande zote mbili. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky amethibitisha kwamba idadi ya vifo vilivyotokea kufuatia shambulizi la roketi lililofanywa katika mji wa Chasiv Yar Jumamosi iliyopita imeongezeka hadi kufikia watu 31.

Zelensky alisema uondoaji wa vifusi uliendelea kutwa nzima juzi mjini Chasiv Yar katika eneo la Donetsk.

Mji wa Kharikiv umeshuhudia mashambulizi mapya ya umwagaji damu yaliyofanywa na jeshi la Russia.

"Kombora lingine lililenga jengo la makazi, lango moja lilibomolewa na kuharibiwa kabisa, washambuliaji walipiga wilaya za Saltiv na Kyiv kwa makombora. Watu watano waliuawawa," alisema Zelensky.

Rais Zelensky alisema amezungumza na waziri mkuu wa Uholanzi Mark Rutte na Rais wa Uturuki HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/mazungumzo-ya-urusi-na-ukraine-kuanza-istanbul/a-61280262" Recep Tayyip Erdogan.

Zelensky amedokeza kuwa amezungumza na Erdogan kuhusu kufungua njia za nchi yake za kuuzia bidhaa nje ya nchi kupitia Bahari Nyeusi. Shirika la habari la Interfax, likiinukuu wizara ya mambo ya nje ya Russia, kwamba duru mpya ya mazungumzo kati ya Russia, Ukraine, Uturuki na Umoja wa Mataifa kuhusu usafirishaji nje wa ngano kutoka Ukraine inatarajiwa kufanyika leo mjini Istanbul.

Wakati hayo yakiarifiwa watu wapatao 12 wamejeruhiwa katika mashambulizi ya makombora katika mji wa kusini wa Mykolaiv usiku wa kuamkia jana.

Gavana wa eneo hilo Vitaly Kim, alisema makombora kadhaa yalivurumishwa katika vituo viwili vya matibabu na majengo ya makazi ya watu.

Kamishna wa Umoja wa Ulaya anayeshughulikia masuala ya sheria, Didier Reyners, alisema umoja huo umezuia mali za Russia za thamani ya dola bilioni 13.8 tangu ilipoivamia Ukraine Februari 24 mwaka huu. **DW**



Watu wakiangalia gari lilobeba mwili wa waziri mkuu wa zamani wa Japan, Shinzo Abe, wakati ukiwasili katika eneo la maziko katika hekalu la Zojoji jijini Tokyo jana. Abe aliuawa kwa kupigwa risasi wakati akihutubia mkutano wa kampeni mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: REUTERS**

# Shinzo Abe aagwa kiheshima

**TOKYO, Japan**

MAELFU ya waombolezaji wamejitokeza kutoa heshima zao za mwisho kwa waziri mkuu wa zamani wa Japan, Shinzo Abe siku ya jana.

Mazishi ya faragha, ambayo yalihudhuriwa na familia na marafiki wa karibu pekee, yalifanyika katika hekalu la Zojoji la Tokyo.

Katika mazishi hayo, gari la kubebea maiti lililobeba mwili wa Abe lilitembea katikati mwa jiji la Tokyo.

Mzee huyo mwenye umri wa miaka 67 aliuawa kwa kupigwa risasi Ijumaa iliyopita alipokuwa akitoa hotuba katika kampeni katika mji wa Nara kusini mwa Japan.

Ndani ya hekalu la Zojoji, ibada za Wabudha zilifanywa na baadae mazishi yalifanyika.

Katika jiji la Tokyo na maeneo mbalimbali ya Japan bendera zinapepea nusu mlingoti.

Msafara wa mazishi Jumanne alasiri utapita kwenye maeneo muhimu kama vile jengo la bunge, ambalo Abe aliingia kwa mara ya kwanza kama mbunge mnamo 1993, na ofisi ambayo aliongoza taifa kama waziri mkuu. **BBC**

# VIONGOZI BIASHARA UNITED WAJIUZULU

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushuka daraja viongozi wa Biashara United wakiongozwa na Mwenyekiti Selemani Mataso wamejiuzulu nyadhifa zao.

Viongozi hao walijiuzulu kwenye Mkutano wa dharula uliofanyika mkoani Mara kwa kile kilichoelezwa ni kushindwa kuwajibika.

"Kwanza tunaomba radhi kwa watu wote wa Mara, lakini mimi nawasihi wajumbe wenzangu katika kikao cha leo kupisha ili wengine nao wao waje kuongoza na sisi tuwape ushirikiano ili tusonge mbele," alisema Mwenyekiti huyo kwenye mkutano huo akiwasilisha hoja hiyo ya wao kujiuzulu, kabla ya kufanya hivyo.

Baadhi ya wanachama kwenye mkutano huo walisema msimu huu wamefeli kwa sababu ulikuwepo uzembe mkubwa sana na kuifanya timu hiyo iliyosimama kama nembo ya mkoa wa Mara kushuka.

Baada ya kufanya hivyo, Mbaraka Forogo alichaguliwa kukaimu nafasi hiyo hadi pale uchaguzi huo utakapofanyika.

"Tunawataka mashabiki wa mkoa wa Mara kuendelea kutuunga mkono ili tuendelee kuiendesha timu kwa ajili ya kuirudisha Ligi Kuu msimu ujao, lakini pia baada ya hili tutafanya kila njia ili uchaguzi ufanyike mapema," alisema Kaimu Mwenyekiti huyo.

Biashara United ambayo msimu uliopita ilipata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye mechi za kimataifa na ikafanya hivyo msimu huu kabla ya kuondolewa baada ya kushindwa kwenda nchini Libya kucheza na Al Ahli Tripoli, msimu huu ilimaliza ikiwa nafasi ya 15, ikishinda mechi tano tu kati ya 30 ilizocheza, sare 13 na kupoteza mechi 12




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga Uwasa) Mhandisi Geofrey Hilly (kulia) akikabidhi vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 2 kwa Ofisa Elimu Msingi Jiji la Tanga, Kasim Kaonekana kwa ajili ya michezo ya Umitashumta iliyoanza jana kwenye Shule ya Sekondari Tanga. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

## Uwasa yakabidhi vifaa vya michezo Tanga Jiji

**Na Oscar Assenga,TANGA.**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga Uwasa) imetoa vifaa vya michezo vyenye thamani ya Milioni 2, kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa ajili ya michezo ya Umitashumta inayofanyika kwenye shule ya Sekondari Tanga.

Halfa ya makabidhiano ya vifaa hivyo ilifanyika jana kwenye ofisi za Mamlaka hiyo ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga Uwasa, Mhandisi Geofrey Hilly alimkabidhi Ofisa Elimu Msingi, Kasimu Kaoneka kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Tanga.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi vifaa hivyo Hilly alisema wameamua kutoa msaada huo ili kuweza kuunga mkono mashindano hayo.

Alisema wao Tanga Uwasa kama wadau wa elimu wanatambua umuhimu wa michezo katika elimu kwa ajili ya wanafunzi ili waweze kupata afya nzuri na kuweza kusoma vizuri.

Alisema wanatambua kuwa mazingira bora yanasaidia kuwa na elimu bora licha ya kuchangia michezo, lakini wanachangia ujenzi wa madarasa na vitu vingine ili kutengeneza mazingira mazuri ya elimu.

Awali akizungumza wakati akipokea vifaa hivyo, Ofisa Elimu Msingi Kaoneka alisema kwamba michezo ni kitu muhimu kwa wanafunzi kwani wanaenda shuleni kupata taaluma.

"Tunawashukuru Tanga Uwasa kwa kutupatia vifaa hivi vya michezo na tunaahidi kwamba tutahakikisha tunaleta vikombe vingi na tutawakaribisha wakati wa kukabidhiwa," alisema

## Yanga Princess kufanya usajili wa nguvu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umewaondoa presha mashabiki wa timu hiyo kwa kuhakikisha kwamba, msimu ujao timu yao ya Wanawake itakuwa imara na kuanza kubeba taji la Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji alisema ndani ya siku hizi mbili atakuwa na kikao cha kamati ya utendaji pia watapitia ripoti ya kocha wa Yanga Princess, Edna Lema kwa ajili ya kuona aina ya wachezaji ambao wanahitaji kusajiliwa.

Alisema muda wa usajili uliobaki ni mchache wanalazimika viongozi kukaa haraka kwa pamoja kuangalia uwezako wa kuboresha timu yao hiyo ya wanawake ila msimu ujao kufikia malengo yao.

"Ukiangalia msimu huu haukuwa mzuri kwa timu yetu ya wanawake ila niwahakikishie wanayanga tunaenda kuboresha timu ya wanawake kuwa tishio na wao kuanza kupata furaha ya kuchukuwa makombe," alisema Arafat.

Alisema tayari mikakati hiyo ipo imara na wanachokifanya sasa ni jinsi ya kuimarisha timu yao ya wanawake ili msimu ujao kupambana na kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

## Azam kuweka kambi siku 20 Afrika Kusini

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa klabu ya Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' amesema timu yao itaweka kambi ya siku 20 Afrika Kusini kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili, kiongozi huyo ameeleza kinachofanyika hivi sasa ni kukamilisha baadhi ya taratibu za kambi hiyo lengo likiwa ni kulipa muda benchi la ufundi kuiandaa timu.

"Hadi sasa kila kitu kipo vizuri usajili tumeshaukamilisha kwa asilimia kubwa, kama itatokea kuna mchezaji tutamuongeza tutaeleza," amesema Popat.

Aidha alisema Azam inatarajia kuanza mazoezi Julai 14 na siku inayofuata itaondoka kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kambi hiyo ambayo ameita kuwa ni ya kurudisha heshima ya klabu.

Mabingwa hao wa zamani wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ni miongoni mwa klabu iliyotumia kiasi kikubwa cha fedha kwenye usajili wa dirisha hili kubwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN WAKOMAA NA JONG

MTENDAJI Mkuu wa Manchester United, Richard Arnold na mkurugenzi wa ufundi, John Murtough wako Barcelona kujaribu kukamilisha usajili wa kiungo Mholanzi Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Manchester Evening News)***

### TIELEMANS, NEVES WASAKWA

KIUNGO wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, wanasakwa na Manchester United iwapo watashindwa kumnasa Frenkie De Jong. ***(Talksport)***

### RAPHINHA FRESH

BARCELONA imekubali kutoa ada wanayotaka Leeds United ya pauni milioni 65 kwa ajili ya kiungo Mbrazil Raphinha mwenye umri wa miaka 25, na kipaumbele cha sasa cha klabu hiyo ya Hispania ni kumuuza Frenkie De Jong kwenda Manchester United. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMGEUKIA GNABRY

CHELSEA inaonekana iko nyuma ya Barcelona kwa sasa kwenye mbio za kumsaka Raphinha ambapo badala yake huenda wakamgeukia winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Serge Gnabry. ***(Mail)***

### DEMBELE SAFI BARCA

MKATABA wa mshambuliaji, Ousmane Dembele pale Barcelona umeisha, lakini nyota huyo mwenye miaka 25 anatarajia kusaini mkataba mpya kusalia Nou Camp utakaokwenda hadi mwaka 2024. ***(Marca)***

### WOLVES YAMKATALIA WHITE

KLABU ya Wolves imekataa ofa ya pauni milioni 25 kwa ajili ya kiungo, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 22 kutoka Everton. ***(Mail)***

### RODON AWANIWA

KLABU ya Fulham iko kwenye mazungumzo na Tottenham Hotspur kuhusu usajili wa mlinzi wa Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### MBABU ATAKIWA

FULHAM wako katika hatua za mwisho za kumsajili mlinzi wa Uswisi, Kevin Mbabu mwenye umri wa miaka 27 kutoka Wolfsburg ya Ujerumani kwa dau linalofikia pauni milioni 5. ***(Evening Standard)***

### AZPILICUETA KIMEELEWEKA

CHELSEA inataka pauni milioni 7 kutoka kwa Barcelona kwa ajili ya mlinzi wake, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32, ambaye ameshakubaliana kuhusu maslahi binafsi na klabu hiyo ya Katalunya. ***(Evening Standard)***

### N'GOLO AGOMBEWA

ARSENAL inachuana na Manchester United katika harakati za kumsajili kiungo wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31. ***(Express)***

### BUSQUETS ATAKIWA MAREKANI

KIUNGO wa Barcelona na Hispania, Sergio Busquets mwenye umri wa miaka 33, anasakwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DEMBELE KUPUNGUZA MSHAHARA BARCELONA

**Mwenyewe akubali kusaini miaka miwili ili kuhakikisha anabakia hapo Katalunya...**

**BARCELONA, Hispania**

OUSMANE Dembele amekubali kupunguzwa kwa mshahara wake mkubwa ili kusalia Barcelona, kwa mujibu wa 90min, huku klabu hiyo pia ikikaribia kumnasa winga wa Leeds United, Raphinha.

Mazungumzo yaliendelea mwishoni mwa juma kwa mikataba yote miwili baada ya 90min kuthibitisha mapema Jumamosi kwamba, hatua zote mbili zilikuwa karibu, na kunatarajiwa kuwa na harakati zaidi katika siku zijazo.

Dembele, ambaye mkataba wake na Barca ulimalizika mwanzoni mwa Julai, amekuwa kwenye mazungumzo ya kusaini mkataba mpya kwa wiki kadhaa, lakini amekuwa akiwaniwa na klabu nyingine moja wapo ikiwa ni Chelsea.

Lakini Mfaransa huyo anatazamiwa kukataa mpango wa kwenda Ligi Kuu England na badala yake atasaini mkataba wa miaka miwili wa kuongezwa pale Camp Nou - ambao mwanzoni utapunguza asilimia 40 ya mshahara wake wa sasa.

Dembele amekubali kupunguza mshahara wake kwa kuamini kwamba, mkataba mpya na uliooreshwa unaweza kuwa mezani msimu ujao wa joto, ambapo inatarajiwa kwamba fedha za Barca zitakuwa bora zaidi.

Kocha mkuu Xavi ameshinikiza klabu hiyo kumbakisha Dembele, lakini hilo halitawazuia Barcelona katika harakati zao za kumnasa Raphinha, ambaye analengwa pia na Chelsea.

Chelsea walikubaliana na Leeds mwanzoni mwa mwezi huu, lakini Raphinha amebakia kulenga kuhakikisha anahamia Katalunya, ingawa hajakataa kuhamia Stamford Bridge wakati wowote.

Barca walikuwa tayari wamekubali kufikia ofa ya Chelsea ya karibu euro milioni 60 bila kujumuisha nyongeza, lakini muundo wa mpango huo - unaozingatia ni wakati gani malipo yangefanywa.

Wakati Dembele sasa amesafiri kwa ndege hadi Hispania, Raphinha, ambaye ameondolewa kwenye ziara ya Leeds ya kujiandaa na msimu mpya nchini Australia, anasubiri kufanya vivyo hivyo - wakala wake Deco tayari ameshafikia makubaliano kwa maslahi yake kibinafsi.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 281,

MECHI KALI
ISMAILY SC
VERSUS
SMOUHA CLUB
1 | 2.46
X | 3.07
2 | 2.92

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WILSHERE KOCHA WA VIJANA ARSENAL



**LONDON, England**

JACK Wilshere ameteuliwa kuwa kocha mkuu mpya wa Arsenal kwa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England alitangaza kustaafu kucheza soka Ijumaa.

Wilshere anaungana na Mehmet Ali, ambaye anachukua nafasi ya kocha mkuu wa kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 21 akijiunga kama msaidizi Januari.

Wilshere alisema: "Ni heshima kubwa kuwa na jukumu hili. Sio siri kuwa ninaipenda klabu hii. Ninapenda kile tunachosimamia na sehemu kubwa ya maisha yangu niliitumia katika chuo hiki, baadhi ya siku bora zaidi za maisha yangu. Hii ni fursa kubwa kwangu na niko tayari. Nina njaa na siwezi kusubiri kuwasaidia wachezaji hawa wachanga kustawi na kuwa bora zaidi.

"Ni hisia maalum kuwa sehemu ya familia ya Arsenal. Haikuniacha, na ingawa nilisonga mbele kwa miaka michache, moyo wangu ulikuwa bado uko Arsenal. Siwezi kungoja kuanza na kuwasaidia wachezaji hawa wachanga kufanikiwa na timu kubwa karibu nami."

Meneja wa Academy, Per Mertesacker aliongeza: "Hizi ni habari njema kwa kila mtu anayehusika katika chuo chetu. Tumefanya mabadiliko mengi chanya katika wiki chache zilizopita na ninaamini kuwa tuna watu bora zaidi hapa wa kuendeleza maendeleo ambayo tumefanya katika miaka ya hivi karibuni.

"Kila mtu anajua jinsi Jack alivyo na shauku kuhusu Arsenal. Anaelewa kile tunachotaka kufikia hapa na alituvutia sana mwaka jana. Anajua ni nini hasa kinachohitajika ili kuendeleza soka katika kikosi cha kwanza. Mehmet pia alituvutia sana miezi sita iliyopita na tulijua kuwa alikuwa mtu sahihi kuchukua jukumu la Vijana wa U-21."

# Pogba: Nasubiri mataji na Juve

**TURIN, Italia**

PAUL Pogba ambaye amejiunga tena na Juventus kwa mkataba wa miaka minne baada ya muda wake kumalizika kule Manchester United, amebainisha kwamba, anasubiri kwa hamu kubwa kushinda tena mataji na timu hiyo.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29 alishinda Serie A mara nne na miamba hao wa Italia kabla ya uhamisho wa rekodi ya dunia wa pauni milioni 89 kwenda United mwaka 2016.

Alisafiri kwa ndege hadi Turin, Ijumaa kwa vipimo vya afya yake kabla ya tangazo la kusajiliwa kwake rasmi Jumatatu.

Pogba aliichezea United mara ya mwisho Aprili 19 kwa sababu ya jeraha, na alikuwa mchezaji huru msimu huu wa joto baada ya yeye na klabu kushindwa kuafikiana kuhusu mkataba mpya.

Klabu hiyo ilithibitisha mwanzoni mwa Juni kwamba, ataondoka Old Trafford msimu huu wa joto.

Katika video kwenye mtandao wa kijamii wa Juventus, Pogba alisema: "Kama unavyoona, nimerudi na nina furaha sana - siwezi kusubiri kuanza na kushinda makombe hapa."

Pogba, ambaye alijiunga na akademi ya United akitokea Le Havre akiwa na umri wa miaka 16 mwaka 2009, aliwasaidia Mashetani Wekundu hao kushinda Kombe la EFL na Ligi ya Europa katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo.

Kutoelewana na kocha wa wakati huo wa United, Jose Mourinho, kulimfanya apoteze umakamu nahodha mwaka 2018.

Pogba, ambaye ana mechi 91 za kimataifa, alikuwa na ushawishi wakati Ufaransa ilishinda Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka 2018.

Aliifungia United mabao 16 katika msimu wa 2018-19, lakini katika misimu mitatu iliyopita alifunga mabao nane katika mechi 91, huku moja kati ya 27 msimu uliopita.

Juventus walimaliza katika nafasi ya nne kwenye Serie A kwa msimu wa pili mfululizo, wakiwa nyuma ya mabingwa AC Milan kwa pointi 16.

Walikuwa mabingwa wa Italia kwa misimu tisa iliyotangulia, huku Pogba akicheza jukumu muhimu katika ushindi wao wa taji kutoka msimu wa 2012-13 hadi 2015-16.

## HABARI MICHEZO


620,910

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/07/22 | 19:30 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.48 | 3.01 | 2.96 |
| 02. 13/07/22 | 20:00 | Dinamo Batumi vs Slovan Bratislava | 2.56 | 3.06 | 2.76 |
| 03. 13/07/22 | 20:00 | Shakhter Soligorsk vs Maribor | 2.66 | 3.06 | 2.66 |
| 04. 13/07/22 | 21:45 | Linfield Belfast vs The New Saints | 2.30 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 14/07/22 | 01:00 | Goias vs Atletico GO | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 06. 14/07/22 | 02:00 | Ceara CE vs Fortaleza CE | 2.41 | 2.85 | 2.99 |
| 07. 14/07/22 | 03:00 | Inter Miami CF vs Philadelphia Union | 2.70 | 3.36 | 2.55 |
| 08. 14/07/22 | 03:30 | Santos vs Corinthians | 2.35 | 2.94 | 2.99 |
| 09. 14/07/22 | 04:00 | FC Dallas vs New York City | 2.53 | 3.57 | 2.60 |
| 10. 14/07/22 | 18:00 | College Europa vs Vikingur Gota | 2.37 | 3.33 | 2.88 |
| 11. 14/07/22 | 18:00 | Ararat Yerevan vs Shkendija | 2.29 | 3.37 | 2.97 |
| 12. 14/07/22 | 19:00 | Milsami Orhei vs FK Panevezys | 2.78 | 3.18 | 2.53 |
| 13. 14/07/22 | 19:00 | Seinajoen JK vs Flora Tallinn | 2.82 | 3.23 | 2.46 |

# MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 13/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2576 | Visakha FC vs Angkor Tiger FC | 1.55 | 4.43 | 4.33 |
| 14:30 | 5828 | Phnom Penh vs National Defense Ministry FC | 1.49 | 4.31 | 5.09 |
| 14:45 | 2302 | Hougang United vs Tampines | 3.09 | 4.22 | 1.85 |
| 16:00 | 2902 | San Lorenzo de Almagro Res. vs Banfield Reserve | 2.56 | 3.20 | 2.51 |
| 17:00 | 1058 | Defensa Y Justicia Reserve vs CA Sarmiento de Junin | 1.89 | 3.33 | 3.68 |
| 17:00 | 2772 | Patronato Reserve vs CA Central Cordoba SE Reserve | 2.55 | 3.09 | 2.60 |
| 17:00 | 2925 | CA Talleres de Cordoba Reserve vs Boca Jrs | 3.59 | 3.34 | 1.92 |
| 17:00 | 3534 | America Mexico U20 vs Deportivo Toluca U20 | 1.65 | 3.68 | 4.51 |
| 18:00 | 1078 | Oppsal IF vs Fyllingsdalen | 2.25 | 4.33 | 2.35 |
| 18:00 | 4460 | South Africa vs Mozambique | 1.42 | 3.82 | 7.45 |
| 18:00 | 4502 | Jippo vs KuPS Akatemia | 1.22 | 5.90 | 9.05 |
| 18:30 | 4370 | FK Tukums 2000/Tss vs Spartaks Jurmala | 3.10 | 3.44 | 2.06 |
| 19:00 | 1828 | Musa Pori vs FC Jazz | 2.31 | 3.84 | 2.46 |
| 19:00 | 1855 | Flora II vs FC Elva | 3.12 | 5.23 | 1.79 |
| 19:00 | 3598 | Sweden W vs Switzerland W | 1.16 | 6.09 | 13.75 |
| 19:30 | 1088 | Stord vs Bjarg | 3.00 | 3.94 | 1.95 |
| 19:30 | 5101 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 19:30 | 5398 | Al Masry Club vs Farco FC | 2.17 | 3.00 | 3.55 |
| 20:00 | 4779 | Dinamo Batumi vs Slovan Bratislava | 2.41 | 3.06 | 2.96 |
| 20:00 | 5197 | Shakhter Soligorsk vs Maribor | 2.60 | 3.00 | 2.75 |
| 21:00 | 1092 | Ferencvaros TC vs Tobol Kostanay | 1.32 | 4.80 | 8.80 |
| 21:00 | 1132 | Capivariano SP U20 vs Gremio Novorizontino SP U20 | 2.56 | 3.30 | 2.46 |
| 21:00 | 1422 | Bragantino SP U20 vs Botafogo SP U20 | 2.65 | 3.34 | 2.36 |
| 21:00 | 1510 | Monte Azul U20 vs Esporte Clube Sao Bento U20 | 1.71 | 3.59 | 4.23 |
| 21:00 | 1596 | FC SKA Brasil SP U20 vs Flamengo SP U20 | 1.77 | 3.43 | 4.12 |
| 21:00 | 1601 | Palmeiras SP U20 vs Penapolense SP U20 | 1.39 | 4.61 | 6.08 |
| 21:00 | 1623 | Ituano FC U20 vs XV De Novembro SP U20 | 3.59 | 3.30 | 1.93 |
| 21:00 | 1694 | Guarani SP U20 vs EC Agua Santa SP U20 | 1.94 | 3.19 | 3.68 |
| 21:00 | 2394 | Ferroviaria SP U20 vs Sao Jose EC SP | 1.23 | 5.50 | 9.63 |
| 21:00 | 3039 | Ponte Preta SP U20 vs Gremio Osasco Audax EC U20 | 2.02 | 3.49 | 3.15 |
| 21:00 | 3280 | Santos SP U20 vs Tanabi EC SP U20 | 1.33 | 4.72 | 7.47 |
| 21:00 | 4989 | Ibrachina FC SP U20 vs CA Assisense SP U20 | 1.25 | 5.48 | 8.41 |
| 21:00 | 5656 | SAO Paulo SP U20 vs Portuguesa Desportos SP U20 | 1.33 | 4.81 | 7.27 |
| 21:00 | 5703 | Desportivo Brasil U20 vs SAO Caetano SP U20 | 1.52 | 3.94 | 5.32 |
| 21:00 | 5812 | Mirassol FC U20 vs Noroeste SP U20 | 1.39 | 4.41 | 6.47 |
| 21:30 | 1343 | CFR Cluj vs Pyunik Yerevan | 1.22 | 5.41 | 13.02 |
| 21:45 | 1043 | Linfield Belfast vs The New Saints | 2.32 | 3.11 | 3.06 |
| 21:45 | 1873 | Aberdeen vs Dumbarton | 1.07 | 8.44 | 21.58 |
| 21:45 | 2483 | Clyde vs Bonnyrigg Rose | 2.20 | 3.48 | 2.80 |
| 21:45 | 2551 | Raith Rovers vs Peterhead | 1.58 | 3.82 | 4.90 |
| 21:45 | 4467 | Arbroath vs Cowdenbeath | 1.05 | 9.86 | 23.67 |
| 21:45 | 5464 | Kilmarnock vs Partick Thisle | 1.76 | 3.53 | 4.02 |
| 22:00 | 1576 | Netherlands W vs Portugal W | 1.29 | 4.89 | 8.22 |
| 22:00 | 2085 | Club Cortulua vs Jaguares de Cordoba | 2.04 | 3.14 | 3.43 |
| 22:00 | 4341 | America De Cali vs Deportivo Pereira | 1.88 | 3.19 | 3.92 |
| 22:00 | 5140 | Enppi Club vs El Gouna | 2.04 | 3.26 | 3.61 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MSUVA ASHINDA KESI KULIPWA SH. BIL 1.6

**Na Saada Akida**

BAADA ya kusubiri kwa miezi 7 hatimaye Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) limeiamuru klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco imlipe nyota wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva Dola za Marekani 700,000 (sawa na zaidi ya Sh1.6 bilioni).

Kwa mujibu wa familia ya Msuva, imemshukuru Mungu kwa kusikia kilio chao juu ya mtoto wao Msuva aliyeishtaki klabu hiyo FIFA kutokana na kushindwa kumlipa fedha za usajili sambamba na malimbikizo ya mshahara hatua iliyomfanya nyota huyo kurejea nyumbani.

Baba wa Mchezaji huyo, Happygod Msuva amenukuliwa akisema kwamba, tangu Novemba mwaka Jana walipoliwasilisha jambo hilo FIFA familia ilifunga kwa maombi na kumlilia Mungu.

"Familia tuliamua kumuachia Mungu hili jambo na haki imetendeka," alisema.

Amesema baada ya kupata taarifa hiyo familia nzima iliangulia kilio cha furaha baada ya kuisubiri haki kwa muda mrefu.

"Yaani sasa hivi hakuna anayeweza kuongea sio Msuva, kaka, Mama wala dada yake wote wanamshukuru Mungu kwa kutenda," amesema.



Timu ya Taifa ya Soka la ufukweni (Beach Soccer) ikiendelea na mazoezi kwenye fukwe za Coco kujiandaa na mchezo wa kufuzu AFCON (BSAFCON) dhidi ya Malawi. **PICHA: TFF**

# Mastraika wa3 Simba hatarini kutemwa

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA watatu wa Simba, Meddie Kagere, Chris Mugalu na John Bocco wako kwenye kikaango kwa sasa, wakijadiliwa nani abaki, aondoke, au waondoke wote kitu ambacho kimezua mjadala mkali miongoni mwa wajumbe wa klabu hiyo.

Habari zilizopatikana toka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa Wajumbe wa Bodi wameonekana kugawanyika, wengine wakitaka mmoja aondoke, wabaki wawili, wengine wakitaka abaki straika mmoja tu, wawili waondoke, lakini pia wapo wanaotaka wote waachwe.

Mastaika hao wote wameshindwa kuibeba timu hiyo msimu uliomalizika na kupokonywa vikombe vyote, tofauti na msimu mmoja nyuma yake, ambapo wote watatu walifunga mabao zaidi ya 40.

Kwa sasa Simba ipo kwenye maboresho makubwa kwenye kikosi chake, ambapo tayari imeshapata mastraika wawili ambao ni Mzambia Moses Phiri kutoka Zanaco ya Zambia na Habib Kyombo kutoka Mbeya Kwanza.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema kuwa wachezaji hao kila mmoja ana uzuri wake.

"Kuhusu nani ataondoka nani atabaki, au wataondoka wote, hilo litaamuliwa kwenye vikao na jinsi makubaliano na mchezaji yatakavyokuwa, lakini hawa wote, kila mmoja ana uzuri wake ambao mwingine hana," alisema Ahmed.

Wakati huo huo, mchezaji Nassor Kapama ambaye alitambulishwa juzi na klabu hiyo amesema amefurahi kujiunga na Wekundu wa Msimbazi kwa sababu ilikuwa ni ndoto yake siku moja.

"Simba ni timu kubwa Tanzania na nje ya nchi. Kwanza nafurahi kwa sababu ni klabu ya ndoto yangu, nawaomba viongozi, mashabiki na wachezaji wenzangu wanipokee ili kufikisha malengo yetu.

Kikubwa ni kushinda mataji tutakayoshiriki, makubwa na madogo ili na mimi nitimize malengo yangu niliyojiwekea ya kutwaa makombe kwenye karia yangu ya soka," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Kagera Sugar na Ndanda FC.

# Michezo

Jumatano Julai 13, 2022
Nipashe



**Msuva ashinda kesi kulipwa Sh. Bil 1.6**




Kocha Mkuu mpya wa Simba, Zoran Manojnlovi (kushoto), akitambulishwa kwa waandishi wa habari na Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, kwenye hoteli ya Serena, Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

# SIMBA KUPAA MISRI KESHO

●●●Ni kwa ajili ya kambi ya wiki nne, leo kushusha usajili wa mchezaji mkubwa, ambao si wa Afrika bali wa dunia...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinatarajiwa kuondoka nchini kesho, kuelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi ya wiki mbili katika mji wa Ismailia, ikiwa ni maandalizi ya msimu wa 2022/23 wa mashindano ya kimataifa na leo watatanguliza usajili wa mchezaji mkubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana wakati wa kumtambulisha kocha wao mpya, Zoran Manojnlovi, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu ya Simba, Ahmed Ally alisema wachezaji wameanza kuwasili jana na wataweka kambi yao rasmi nchini Misri.

Alisema wachezaji wote waliosajiliwa ndani ya klabu hiyo pamoja na Kocha wao, Zoran wataambatana kwenda nchini humo kasoro wale ambao watakuwa katika majukumu ya kutumikia timu za mataifa yao.

"Wachezaji wote waliosajiliwa watakwenda Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya na kikosi kitarejea nchini Agosti 5, kwa ajili ya sherehe zetu za Simba Day na baadae tunaendelea na maandalizi ya mchezo wetu wa ngao ya Jamii," alisema Ahmed Ally.

"Kwenye usajili kesho (leo) tutaendelea kwa kushusha mchezaji mkubwa. Huu sio usajili wa Afrika bali wa dunia na itasimama," aliongeza Ally.

Alisema ana matarajio makubwa na kocha huyo kwa sababu amewahi kupata mafanikio katika klabu alizopita na kufikia malengo waliyompa katika mkataba ikiwemo kutwaa mataji yote matatu ya ndani na kufikisha Simba nusu fainali ya Afrika.

Katika hatua nyingi, Zoran alisema amesaini mkataba wa mwaka mmoja kukinoa Simba na ni muda mchache lakini ana imani kuwa unatosha.

Alisema katika soka na mfumo wake unahitaji kupata muda wa miezi minne ila kutokana na kulifahamu soka la Afrika ana imani muda unatosha kufikisha yale ambayo wamekubaliana katika mkataba wake.

"Nimekuja kufanya kazi na kuhakikisha nafikia malengo ya Simba, kwa kushinda mataji yote ya ndani na kufikisha nusu fainali ya Afrika," alisema.

"Nipo hapa kuifanya Simba kuwa bora zaidi ya msimu uliopita. Mwaka huu ilimaliza nafasi ya pili, msimu ujao inatakiwa kuwa ya kwanza, msimu uliopita ilikuwa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika na mwaka huu kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kwa muda ambao tunaenda 'Pre Season' unatosha kuwanoa wachezaji. Nina taarifa kuhusu usajili wote ambao umekuwa ukifanywa na uongozi kwa ajili ya msimu mpya. Nimepata mafanikio katika timu mbalimbali ambazo nimewahi kufanya kazi. Simba ni timu kubwa Tanzania, ni changamoto kubwa kwangu kwa mafanikio waliyopata Afrika hivyo kuna kazi ya kufanya.

"Sina hofu juu ya soka la Afrika kwa sababu ya nchi nne nilizofundisha ikiwemo Angola, Algeria, Morocco na Sudan nilipata mafanikio."

Zoran amesaini mkataba wa mwaka mmoja, lakini una kipengele cha kuongeza kama akifikia malengo."

## Yanga yamaliza usajili wa CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema usajili inaoufanya sasa umelenga kufanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku ikiweka wazi kuwa imemaliza usajili wa wachezaji kwa ajili ya michuano ya kimataifa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema baada ya juzi kutambulisha usajili wa beki wa kushoto Joyce Lomalisa kutoka CD Sagrada Esperanca ya Angola, jana usiku saa sita ilitarajia kumtambulisha mchezaji mwingine ambaye imesema atakuwa wa mwisho msimu huu na tayari maandalizi yataanza kwa ajili ya michuano ya kimataifa na mashindano mengine ya msimu.

"Mchezaji wa mwisho naye ameshafika. Alifika usiku, saa tisa au kumi, sasa kama atasema anapumzika, hatutamtangaza, lakini kama mambo yatakwenda vema tunamtangaza leo saa sita usiku (jana) hatutobadilisha muda, ndiyo ambao tumejipangia wenyewe," alisema Bumbuli.

Tayari Yanga imewatambulisha wachezaji watatu, huku jana ikitarajia kumtangaza wa nne.

Wachezaji hao wote wa kimataifa ni Lazarous Kambole raia wa Zambia na Gel Bigirimana kutoka Burundi, kabla ya kumsajili Lomalisa ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Bumbuli alibainisha lengo la usajili ni kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa na kuwa washindani zaidi.

"Katika ligi ya ndani hatujabadilisha sana kikosi. Hiki kilichotwaa mataji matatu kipo na kinaweza kucheza na timu yoyote ya hapa nchini na kikapata ushindi, lakini kwa Ligi ya Mabingwa. Lengo letu tunahakikisha kufanya vizuri. Tutafika wapi tunamuachia Mwenyezi Mungu, tunataka kuwa washindani, ndiyo maana viongozi wameamua kuwaleta wachezaji wa kimataifa, kwa sababu wengi wana uzoefu wa michuano hiyo," alisema Bumbuli.

Yanga imeonyesha haitaki masihara kuelekea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa msimu ujao kutokana na jinsi inavyoonekana kujiandaa baada ya msimu uliopita kuondolewa kwenye hatua za awali kwa kufungwa mabao 2-0, bao 1-0 nyumbani na ugenini dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >